KISWAHILI



LUGHA YA KUFUNDISHIA KIKWAZO CHA USAWA KATIKA KUJIFUNZA NA UPIMAJI TANZANIA

KISWAHILI KICHOCHEO CHA KUKUZA FIKRA TUNDUIZI NA UBUNIFU

Wahariri
Wilberforce E. Meena na John Kalage

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 1 06/07/2023 12:15 PM

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 2 06/07/2023 12:15 PM

Yaliyomo

1.	Dibaji *Rwekaza Sympho Mukandala.*	**2**
2.	Usuli *John Kalage.*	**4**
3.	Tafakuri ya Jumla: Kiswahili Kitumike Kuimarisha Usawa katika Kujifunza na Upimaji *Wilberforce E Meena.*	**6**
4.	'Gogo la Mti Lijapowekwa Mtoni Miaka 100 Haliwezi Kugeuka Mamba' Tutumie Kiswahili kuwa Lugha ya Utambulisho na Kukuza Maarifa *Aldin K. Mutembei.*	**11**
5.	Kiswahili ni Lugha ya Taifa: Kwa nini sio Lugha ya Kufundishia? *Humphrey P. B. Moshi.*	**22**
6.	Kuboresha Ufundishaji wa Kiingereza Katika Shule za Sekondari Tanzania: Umuhimu wa Kuzingatia Maelekezo ya Nadharia *Martha Qorro.*	**27**

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 1 06/07/2023 12:15 PM

Dibaji

Kama Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, bado angekuwa hai, basi angetimiza miaka 100 mwaka 2022. Mwalimu Nyerere alifariki dunia mwaka 1999. Hata hivyo, mawazo na mchango wake mkubwa kwa Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla bado unakumbukwa na kuthaminiwa ndani na nje nchi. Heshima kubwa aliyojijengea imepelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Kigoda cha Kiprofesa cha Mwalimu Nyerere katika Umajumui wa Afrika, kuandaa makongamano yanayohusiana na falsafa, fikra na mchango wa Mwalimu karibu kila mwaka. Mwaka 2022 Kigoda kiliandaa kongamano ili kusherehekea miaka 100 ya kuzaliwa kwa Mwalimu, na watu mbalimbali waliwasilisha makala zilizosheeni maarifa na mawazo mazuri.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa makala zinazohusu Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia ambazo ziliwasilishwa katika kongamano hilo. Wakati wa uhai wake, Mwalimu Nyerere aliitambua nafasi adhimu ya Kiswahili katika Taifa la Tanzania kwa ujumla na hususan katika nyanja ya elimu, ndiyo maana mwaka 1967 alikipa Kiswahili hadhi ya kuwa Lugha ya Taifa na kuamuru kitumike kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na kifundishwe kama somo katika ngazi zote za elimu nchini. Pia aliamuru Kiingereza kiendelee kutumika kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuoni, vikiwamo vyuo vikuu. Katika ngazi hizi mbili za elimu Kiswahili kinafundishwa kama somo tu.

Kwa muda mrefu watafiti wameonesha athari za kuendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunzia, ikizingatiwa kwamba sio wanafunzi wala walimu wanaimudu lugha hiyo. Kwa mfano, wameonesha kwamba Kiingereza hakitoi mwanya kwa watoto wa Watanzania kuwa wabunifu na kwamba kinaua vipaji vyao. Makala ya Meena, ambayo imo katika kitabu hiki, inaonesha kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza yanaondoa usawa katika ujifunzaji na upimaji. Makala hiyo inadai kuwa wanafunzi wa sekondari wanaotoka katika shule za msingi za umma wanafanya vibaya zaidi katika eneo la ujifunzaji na upimaji kuliko wale wanaotoka katika shule za msingi za binafsi zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Sababu ya hali hii ni kwamba wanafunzi wanaotoka katika shule za msingi za umma wana umahiri duni katika Kiingereza. Meena anabeua dai kwamba Kiswahili kinajitoshelezi kama lugha ya kufundishia na kujifunzia, kwani lugha hiyo ina msamiati wa kutosha na sifa zingine nyingi. Hivyo anapendekeza vitabu ambavyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliviandika kwa Kiswahili vitumike kwenye baadhi ya shule za sekondari ili kuona hali itakuwaje, pamoja na kubaini changamoto zitakazojitokeza.

Hoja kuhusu athari ya kuendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia inaungwa mkono na Aldin Mutembei. Mutembei anaeleza kuwa Kiingereza kinaua ndoto za watoto wa Tanzania. Anasema kwamba gogo la mti haliwezi kugeuka mamba hata kama litakaa mtoni miaka 100. Kauli hii maana yake ni kwamba hata kama Kiingereza kitaendelea kutumika kama lugha ya kufundishia na kujifunzia watoto wa Tanzania hawatakimudu kamwe. Mutembei anadai pia kwamba matumizi ya Kiingereza yanaifanya elimu iwe ufunguo wa kuyafunga maisha ya watoto wa Tanzania, badala ya kuwa ufunguo wa kuyafungua. Hivyo anapendekeza utekelezaji wa sera ya elimu ya mwaka 2014 mara moja.

Humphrey B. Moshi anaonesha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu nchini kwani kina msamiati wa kutosha na kimepiga hatua kubwa kwenye nyanja za uchumi, teknolojia na nyinginezo ambako kinatumika sana. Maendeleo haya yanamfanya mwandishi ashangae ni kwa nini serikali hairuhusu Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu.
Makala ya Martha Qorro inaangalia ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa Qorro, kuna matatizo makubwa mawili kwenye ufundishaji wa Kiingereza nchini. Moja ni kwamba nadharia za ufundishaji lugha hazizingatiwi. Hivyo haijulikani Watanzania wanajifunza Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni. Tatizo la pili linahusu sera ya elimu, ambayo haizingatii

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 2 06/07/2023 12:15 PM

mazingira ya mawasiliano ya jamii ya Tanzania katika kuamua ni lugha ipi itumike kufundishia. Vilevile Qorro anadai kuwa Kiingereza hakifundishwi vizuri na vitabu vinavyotumika kufundishia lugha hiyo haviendani na ngazi mahususi ya elimu. Hoja ya msingi ya Qorro ni kwamba Kiingereza kikifundishwa vizuri Watanzania watajenga umahiri wa kutosha, hata kama hakitumiki kama lugha ya kufundishia.

Mwisho, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa waandishi wa makala zote nne zilizomo katika kitabu hiki kwani makala hizo ni mchango muhimu kwenye mjadala juu ya mustakabali wa taifa letu, ikizingatiwa kwamba zinahusu lugha ya kufundishia na kujifunzia. Kama asemavyo Mutembei, kuna mnasaba mkubwa baina ya lugha na elimu. Hali kadhalika, tunawashukuru wale wote waliowezesha kongamano kufanyika kwa kutoa mchango wao wa hali na mali. Hasa hasa, tunakishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Uongozi na HakiElimu kwa ufadhili walioutoa.

Rwekaza Sympho Mukandala
Nyagoda, Kigoda cha Kiprofesa cha Mwalimu J.K. Nyerere katika Umajumui wa Afrika, na
Makamu Mkuu Mstaafu,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

© HakiElimu 2023
ISBN 978-9987-18-083-7

Sehemu yoyote katika kitabu hiki inaweza kutolewa kwa namna nyingine yoyote kwa madhumuni ya kielimu na yasiyo ya kibiashara, kwa kuzingatia kuwa chanzo kitatajwa.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 3 06/07/2023 12:15 PM

Usuli

John Kalage
HakiElimu

Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa tunapojadili maendeleo ya elimu tuhakikishe kuwa ina thamani kwenye ngazi ya kidunia na nchi. Hii ina maana kuwa, ni muhimu kuwajengea wanafunzi maarifa, stadi na mwenendo utakaowawezesha kuishi katika ulimwengu unaobadilika sambamba na kuwa na maarifa ya mila, desturi na utamaduni utakaowatambulisha kama Waafrika na Watanzania. Lugha ya Kiswahili ni moja ya utambulisho wa Mtanzania ambayo kwa sasa imepewa hadhi kubwa kimataifa kwa kutengewa siku maalumu ya maadhimisho ya Kiswahili, ambayo ni tarehe 7 Julai kila mwaka. Kiswahili ndio lugha inayotumiwa na watanzania wengi katika maisha yao ya kila siku, na hivyo ni rahisi kwa wanafunzi kuitumia katika kujifunza[1] . Hivyo, ilikuwa ni fursa ya kipekee kwa HakiElimu kushirikiana na Kigoda cha Mwalimu kuandaa tamasha hii la kumbukumbu ya miaka 100 ya kuzaliwa Mwalimu Julius Nyerere na kuendeleza mjadala wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia. Kiswahili kina nafasi kubwa katika kukuza fikra tunduizi, uvumbuzi, stadi za kutatua matatizo na utambulisho wa Mwafrika.

Pamoja na kwamba, Kiswahili ni utambulisho wa Watanzania hakitumiki kufundisha katika ngazi zote za elimu, jambo ambalo limeibua mjadala kwa muda mrefu ambao una makundi mawili. Kundi la kwanza linapendekeza Kiswahili kitumike kufundishia kuanzia elimu ya awali mpaka elimu ya juu. Kundi la pili linapendekeza hali iendele ilivyo ambapo Kiingereza kinatumika kufundisha katika elimu ya sekondari na elimu juu. HakiElimu tangu kuanzishwa kwake imekuwa ikiendesha kampeni ya kutumia Kiswahili kufundishia kwenye ngazi zote za elimu ili kuwezesha wanafunzi kujifunza na kukuza umahiri unaokusudiwa. Tafiti, zinaonesha kuwa wanafunzi hawaelewi vya kutosha wanachojifunza kutokana na uwezo mdogo kwenye lugha ya Kiingereza (Qorro, 2006). Na kwa mujibu wa Brock-Utne (2004) Kingereza hakitumiki vizuri kama lugha ya kufundishia.

HakiElimu haipingi matumizi ya Kiingereza ila kwa sababu Kiswahili ndiyo lugha inayotumiwa kila siku na Watanzania walio wengi, kitawawezesha wanafunzi kujifunza kwa ufanisi, kwa sababu wataweza kuuliza na kujibu maswali wanapokuwa darasani. Hali kama hii, ilijitokeza wazi kwenye mijadala ya tamasha ambapo baadhi ya wachangiaji walioomba au waliamua kutumia lugha ya Kiswahili kwenye makala ambazo ziliwasilishwa kwa lugha ya Kiingereza. Sasa hivi, kwenye mikutano na makongamano mengi yanayofanyika lugha zote mbili zinatumika. Tena, wakati mwingine mkutano unaweza kuanza kwa Kiingereza na baada ya muda mfupi ukatawaliwa na Kiswahili. Watanzania wanajiachia vya kutosha wanapotumia Kiswahili.

Napenda kuwashukuru sana waandishi wa makala za kitabu hiki ambao kama sio wao kitabu hiki kisingeandikwa. Aldin Mutembei katika makala yake anathibitisha kuwa Kiswahili kinaweza kutumika kufundisha katika ngazi zote za elimu, kilichobaki ni utekelezaji tu. Humphrey P. B. Moshi anatumia uzoefu wake kama mchumi kuonesha jinsi Kiswahili kinavyotumika kwenye maandiko mengi ya kitaifa, kwa hiyo hakuna sababu ya kuwa na hofu ya kukitumia kwa sababu kimejitosheleza kihisitilahi.

Kama nilivyosema awali, HakiElimu tunaunga adhama ya Serikali kuendeeleza matumizi ya lugha ya Kiingereza, Alama, pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo[2] . Martha Qorro katika makala yake anaonesha wazi kuwa Kiingereza hakifundishwi ipasavyo, hivyo anapendekeza mbinu za kuboresha ufundishaji wake.

---

[1] Qorro M (2006). Does Language of Instruction Affect Quality of Education? Dar es Salaam: HakiElimu.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 4 06/07/2023 12:15 PM

Lengo la kitabu hiki ni kuendeleza mjadala na kupendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili wanafunzi wajifunze kwa mafanikio. Katika mpango mkakati wa HakiElimu (2022-2026)[3] tumebainisha wazi kuwa matumizi ya Kiingereza kufundishia kwenye elimu ya sekondari kunasababisha kukosekana usawa katika kujifunza. Wilberforce Meena anafafanua dhana ya usawa katika kujifunza na upimaji kwenye tafakuri ya jumla ya kitabu hiki. Ni wazi kwamba, usawa katika elimu utaimarika kama wanafunzi wote wanaweza kujifunza badala ya wengine kuwa wahudhuriaji tu, kutokana na uwezo mdogo kwenye lugha inayotumika kujifunzia na kufundishia.

Ni mategemeo yangu kuwa, tunapotafakari kuhusu miaka 100 ya mwalimu Nyerere, tunatakiwa kujiuliza kama elimu yetu ina thamani kwa wale wanaoipata. Mchango wa Mwalimu kwenye lugha ya Kiswahili unafahamika, huu ni wakati wetu kuendeleza pale alipoishia. Kiswahili kinaweza kutumika kufundishia ili mradi tuwe na mpango mzuri wa utekelezaji, vifaa na walimu wenye umahiri unaohitajika. Tushirikiane wote kuhimiza matumizi ya Kiswahili na ufundishaji unaofaa wa Kiingereza.

Asante sana.

[2] Wizaya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WyEMU). (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo.* Dar es Salaam, Tanzania:
[3] HakiElimu (2022). *The Strategic Plan. Our Education. Our Future. The Pathway to the Education. We Want.* Dar es Salaam: HakiElimu.

Marejeo

Brock-Utne, B. (2004). English as the language of instruction or destruction – how do teachers and students in Tanzania cope? In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai & Martha Quorro (eds). *Researching the language of instruction in Tanzania and South Africa.* Cape Town: African Minds.
Qorro, M. (2006). *Does Language of Instruction Affect Quality of Education?* Dar es Salaam: HakiElimu.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 5 06/07/2023 12:15 PM

Tafakuri ya Jumla: Kiswahili Kitumike Kuimarisha Usawa katika Kujifunza na Upimaji

Wilberforce E. Meena
HakiElimu

Utangulizi

Usawa katika kujifunza hautaweza kufikiwa kama wanafunzi wanajifunza kwa lugha ambayo hawaielewi na hawaitumii katika maisha yao ya kila siku (HakiElimu, Mpango Mkakati 2022-2026). Hata hivyo, usawa katika elimu umekuwa unaelekezwa zaidi katika uandikishaji, jinsia na elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu na mahitaji maalumu (WyEMU, 2014). Matamko kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 ni kama ifuatavyo:

> **Tamko** 3.3.1. Serikali itaendelea kuongeza fursa anuwai za elimu na mafunzo kwa usawa kwa makundi yote ya kijamii katika ngazi zote ikiwemo watoto wenye mahitaji maalumu (WyEMU Uk 42)

> **Tamko** 3.3.3. Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kuwa usawa wa kijinsi katika elimu na mafunzo unazingatiwa (WyEMU Uk. 43)

Kwenye eneo la lugha sera inasitiza kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni sambamba na lugha ya alama. Mtazamo huu wa Serikali, haubainishi moja kwa moja uhusiano wa lugha na usawa katika elimu. Katika tafakuri hii, nitafanya uchambuzi wa kina kuhusu jinsi lugha ya kufundishia inavyochangia kukosekana kwa usawa katika kujifunza na upimaji. Mwisho, nitaibua hoja ambazo majibu yake yanaweza kutoa mtazamo mpya kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari na elimu ya juu, pamoja na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa Kiingereza.

Lugha ya Kufundishia na Mzunguko wa Kukosekana Usawa katika Kujifunza

Hali ilivyo sasa ni kwamba katika elimu ya sekondari wanafunzi hawajifunzi kwa usawa. Wanafunzi wanaotoka shule za msingi

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 6 06/07/2023 12:15 PM

za serikali zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia na familia zenye kipato cha chini wana uzoefu mdogo kwenye lugha ya Kiingrereza na hivyo wanashidwa kujifunza kwa ufanisi. Hii inamaanisha kuwa wananyimwa fursa ya kujifunza kwa kina na wanaishia kujifunza kipurure. Brock-Utne (2007) anasisitiza kuwa njia za kufundisha zinazomlenga mwanafunzi kama kitovu cha kujifunza hazitaweza kufanikiwa kutokana na kikwazo cha lugha kwa wanafunzi na walimu. Wapo wanaoweza kusema kuwa mbona lugha ya Kiswahili inatumika katika shule za msingi na bado wanafunzi wanamaliza elimu ya msingi bila ya kuwa na kiwango cha kutosha cha stadi muhimu. Hata hivyo, ni wazi kwamba mafunzo ya ualimu hayawafanyi walimu kuwa na umahiri wa kutosha kwenye maudhui ya masomo kutokana na changamoto ya lugha kwenye vyuo vya ualimu na vyuo vikuu.

Walimu wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya astashahada kwa elimu ya msingi, wanajifunza kwa Kiswahili badala ya Kiingereza kinachotumika kwenye elimu ya sekondari. Ni dhahiri kwamba kubadilika kwa lugha kunasababisha ugumu katika kujifunza kwao kama vyuo vya ualimu havijaandiliwa vizuri. Msanjila (2010) anabainisha kuwa matumizi ya Kiswahili kufundisha katika vyuo vya ualimu yanakosa ufanisi kwa sababu wakufunzi hawajaandaliwa vya kutosha kufundisha kwa Kiswahili na pia kuna changamoto ya usambazaji wa istilahi.

Uzoefu kwenye vyuo vya ualimu unaonesha kuwa wakufunzi huwa wanachanganya lugha pale wanapojaribu kuelezea dhana ambayo walijifunza kwa Kiingereza. Hali hii, inasababisha walimu wanafunzi kushidwa kujifunza kwa kina kwa lugha ya Kiswahili mtaala wa mafunzo ya ualimu. Katika hali hii, Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 (Uk 3) imeweka wazi kuwa kuna tatizo la walimu na wanafunzi kutomudu lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali za elimu.

Mtaala wa ualimu una maeneo makuu manne: Maarifa ya masomo yanayofundishwa shuleni, Njia za Kufundisha, Pedogogia (Masomo ya Ualimu kama mitaala na saikolojia) na Mazoezi ya Kufundisha (Osaki, 2001). Kwa mfano, eneo la masomo ya kufundisha linalenga maudhui ya masomo ya shule ambayo walimu wanafunzi wanapaswa kuyaelewa kwa kina kwa lugha ya Kiswahili ili waweze kuwawezesha wanafunzi wao. Matarajio ni kwamba wakufunzi hawatatumia muda mwingi kufundisha maudhui ya masomo kwa sababu yanafundishwa sekondari. Na kwamba msisitizo utakuwa njia za kufundishia. Hata hivyo, tafiti zinaonesha wazi kuwa wanafunzi wengi wa ualimu wana uwezo wa chini wa maudhui ya masomo pamoja na kwamba wamejifunza kwenye elimu ya sekondari (Kitta, 2004). Kwa bahati mbaya hakuna vitabu vingine vilivyoandikwa kwa Kiswahili ambayo vitawasaidia walimu wanafunzi kuongeza maarifa kwenye masomo wanayofundisha. Vitabu vinavyotumika ni vya kiada ambavyo wakati mwingine vipo kama nukuu ya kufundishia au mwendelezo wa muhtasari.

Vitabu vingi vya pedagogia vinavyotumiwa na wakufunzi vimeandikwa na waandishi wa nje ya nchi na vipo kwenye lugha ya Kiingerezea. Wanachofanya wakufunzi ni kutafsiri kwa Kiswahili wanapofundisha. Lewin na Stuart (2003) wanabainisha kuwa sehemu kubwa ya vitabu na tafiti zilizochapishwa vinatoka kwenye nchi zilizoendelea na vinakuwa na mitazamo ambayo wakati mwingine haiendani na hali halisi ya muktadha wa Afrika. Katika miaka 80 na 90 kulikuwa na jitihada kubwa ya kuandika vitabu vya pedagogia kwa Kiswahili kitu ambacho hakijitokezi sana kwa sasa. Kwa upande mwingine taarifa nyingi za tafiti za elimu ambazo zimefanywa na Watanzania zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hata zile zinazohusu elimu ya msingi. Hali hii, inadhihirisha wazi kuwa walimu wa shule ya msingi hawana wigo mpana wa kujifunza kupitia maandiko.

Umahiri katika Lugha Kizingiti cha Kubaini Uwezo Halisi wa Mwanafunzi kwenye Upimaji

Pamoja na uwezo mdogo wa lugha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi, upimaji kwenye elimu ya sekondari na vyuo vikuu unafanywa kwa Kiingereza. Uhalali wa upimaji unakuwa wa mashaka kwa sababu wanafunzi hawaifahamu lugha inayoutumika (Stobart, 2005). Utafiti uliofanyika katika nchi ya Sweeden unaonesha kuwa walimu wanapowapima wanafunzi kwenye maudhui hawatumi lugha kama kigezo, ingawa wanasisitiza kuwa wanafunzi wanapaswa kutumia lugha kubainisha uwezo wao wa kufikiri kiyakinifu (Reierstam, 2020). Hata hivyo, walimu waliweka wazi kuwa kwenye upimaji wanajielekeza zaidi kwenye dhana za masomo kama inavyojitokeza Tanzania.

Kwenye kusahihisha kazi za wanafunzi, walimu wanaridhika pale mwanafunzi atakapoweza kubainisha dhana za mada husika hata kama hana maelezo ya kutosha. Hali hii haishangazi kwa sababu jamii imekuwa ikihoji kwamba wahitimu wengi wa sekondari na hata vyuo vikuu wanashidwa kujieleza kwenye mahojiano kwa lugha ya Kiingereza na hata kuandika barua za kuomba kazi. Kinachojitokeza wazi ni kwamba, usahihishaji haulengi kuwawezesha wanafunzi kukuza lugha na uandishi unaozingatia ufasaha

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 7 06/07/2023 12:15 PM

wa lugha na kanuni za uandishi. Uzoefu unaonesha kuwa wanafunzi wengi wanapewa alama kwenye insha wanazoandika bila ya kupewa maelezo yoyote.

Baadhi ya walimu kutokana na utafiti uliofanyika Sweeden wanawaruhusu wanafunzi kueleza jambo kwa lugha wanayoifahamu kati ya Kiingereza na Kiswidishi au wanachanganya lugha zote wakati wa utahini (Reierstam, 2020). Hali hii inajitokeza pale mwanafunzi anapojifunza maudhui ya masomo na lugha kwa wakati mmoja. Kwa sababu lengo la upimaji ni kutambua uwezo halisi wa mwanafunzi kwenye eneo husika, walimu wanashawishika kumruhusu mwanafunzi kutumia lugha anayoifahamu vizuri au ambayo yupo huru zaidi kuitumia. Ili kuwatendea haki watahiniwa wakati umefika kuruhusu wanafunzi kuchagua lugha watakayoitumia kwenye mitihani yao.

Ni muhimu kukubali ukweli kwamba wapo wanafunzi ambao mitihani ya kitaifa ni halali kwao kutokana na aina ya shule wanazosoma. Hizi ni shule ambazo zina walimu wa kutosha, vifaa na zana za kujifunza na kufundishia na miundo mbinu ambayo inaifanya shule kuwa rafiki kwa wanafunzi. Katika shule za aina hii wanafunzi wanakamilisha mihitasari ya masomo yao. Zipo shule nyingine ambazo wanafunzi wanakamilisha sehemu tu ya mihitasari ya masomo kutokana na shule kukosa viwezeshi muhimu vya kujifunza. Ukichanganya na uwezo mdogo kwenye lugha ya Kiingereza ni wazi kuwa mitihani ya kitaifa inakosa udhabiti kwa aina hii wanafunzi.

Ujumuishi Usio na Wanafunzi wenye Ulemavu

Kuna jitihada kubwa katika Tanzania ya kuwa na mfumo wa elimu ambao utawawezesha wanafunzi wenye ulemavu kusoma na wenzao kwenye madarasa ya kawaida. Hata hivyo, kama wanafunzi wenye ulemavu hawawezi kuwasiliana na wenzao au wana uwezo mdogo kwenye lugha inayotumika itakuwa sio rahisi kwao kujifunza katika darasa jumuishi[4]. Mikakati ya kitaifa ya elimu Jumuishi inatambua kuwa uzoefu wa awali wa lugha unasababisha wanafunzi wenye ulemavu wa aina fulani (kwa mfano Viziwi) kushidwa kujifunza wanapojiunga na elimu awali, msingi au sekondari. Kwa ujumla, mabadiliko ya lugha yana athari hasi kwa wanafunzi wenye ulemavu wanapojiunga na elimu ya msingi hasa kama Kiswahili sio lugha ya kwanza na kwa shule za sekondari. kama wamehitimu kwenye shule za msingi zinazotumia Kiswahili kufundishia.

Kwa bahati mbaya, wanafunzi ambao hawafahamu Kiswahili hawasaidiwi vya kutosha wanapoanza elimu ya awali au msingi[5] Ili kuwawesha kujifunza wanafunzi ambao Kiswahili sio lugha ya kwanza, ni vyema kuhakikisha kuwa wanafundishwa na walimu wanaofahamu lugha yao ya mama (Kwa mfano India wana utaratibu wa kutumia walimu wanaofahamu lugha ya kwanza au lughamama au wenyeji wa eneo husika kwa madarasa ya awali)[6]. Uratibu huu unaweza kutumika Tanzania kwa wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Hoja ambayo inaweza kuibuliwa ni kuendeleza au kuibua hisia za ukabila, ingawa inakosa nguvu kwa sababu wapo walimu wazawa kwenye maeneo husika na wanafundisha. Kwa upande wa elimu ya sekondari hakuna utaratibu maalumu wa kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kukuza uwezo wao kwenye lugha ya Kiingereza.

Kama ilivyo kwa wanafunzi wengine, upimaji na utahini hauzingatii lugha ambayo mwanafunzi anauwezo nayo. Katika Tanzania mitihani ya kuandika ndiyo kigezo kikubwa cha utahini, kwa hiyo uwezo wa kujieleza kwa maandishi utamwezesha msahihishaji kutoa daraja ambalo litaonesha utendaji wa mwanafunzi. Wakati wa kuandaa mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa 2021/22-25/2026, majadiliano makubwa yalijitokeza kuhusu utahini wa wanafunzi viziwi kwa sababu wana shida katika kutumia viunganishi na vihisishi kwenye uandishi. Mjadala pia uliwagusa wanafunzi wenye usonji, ulemavu wa akili na wale wenye ulemavu wa uziwi na uoni. Pamoja na kwamba, kuna wito wa kutumia zana za aina mbalimbali katika upimaji kama vile hojaji, uchunguzi makini na ufuatiliaji wa utendaji wa kila siku wa mwanafunzi bado suala la lugha linahitaji kupewa kipaumbele. Kwa maneno mengine, mjadala wa lugha ya kufundishia na upimaji unapaswa kuwa ajenda muhimu katika utekelezaji wa elimu jumuishi. Hapa ni muhimu kukumbuka kwamba, wapo wanafunzi ambao wanajifunza kwa lugha ya alama na mguso ambao mabadiliko ya lugha yanaweza kuwa na athari hasi kubwa kwao kama hawatakuwa wameandaliwa vizuri au watakosa walimu na wawezeshaji wenye umahiri unaohitajika.

[4] MoEST. (2022). National Strategy on Inclusive Education 2021/22-25/2026.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 8 06/07/2023 12:15 PM

Hatua za Kuchukua ili Kiswahili kiwe Lugha ya Kufundisha Ngazi Zote za Elimu

Makala za kitabu hiki zimependekeza hatua madhubuti zinazoweza kuchukuliwa ili kufanikisha azma ya kukitumia Kiswahili kama lugha ya kujifunzia na kufundishia katika elimu ya sekondari na juu. Pamoja na mapendekezo yaliyotolewa, kuna hoja ambazo tunapaswa kuzijibu:

Hoja ya kwanza: Kwanini Kiswahili kinatumika kujifunza kwenye mafunzo ya ualimu wa shule za msingi ngazi ya astashada lakini hakitumiki kwenye ngazi nyingine kama stashahada na shahada za ualimu wa shule za awali na msingi? Sera ya Elimu ya 1995 imeweka wazi kuwa lugha ya kufundisha katika vyuo vya ualimu itafanana na ile ya ngazi ya elimu ambayo mhitimu anaandaliwa kufundisha[7]. Mwaka 2015 serikali ilianzisha stashahada ya elimu ya awali na msingi ambapo lugha ya kufundisha ilikuwa Kiswahili. Kwa bahati mbaya kozi hizi hazikuwa endelevu na hata jaribio la kuzirejesha mwaka 2020 halikufanikiwa, hata hivyo bado zinahitajika kwasababu walimu wanatakiwa kujiendeleza wakati wote. Kutolewa kwa mafunzo ya stashahada kwa Kiswahili kutakuwa chachu ya kutoa mafunzo ya shahada ya ualimu wa elimu ya awali, msingi na maalumu kwa lugha ya Kiswahili.

Hoja ya pili: Ili kuwandaa vijana kuipenda na kuithamini nchi yao, somo la Uraia lilibadilishwa mwanzoni mwa miaka ya 70 na kuwa Siasa na lilifundishwa kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi 1992 kulisababisha somo la Uraia kurudishwa na tangu wakati huo linafundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Maudhui ya somo la Siasa yalikuwa yameegemea kwenye mfumo kwa chama kimoja na siasa ya ujamaa na kujitegemea hivyo ilikuwa ni lazima kuwa na somo linaloakisi mfumo wa vyama vingi. Swali la kujiuliza ni kwanini lugha ilibadilika (Brock-Utne, 2002)? Ili kuwafanya vijana wa Kitanzania kuipenda na kuifahamu nchi yao ni vyema somo la Uraia na msomo mengine yanayohusiana na utamaduni wa Kitanzania yakafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Hoja ya tatu: Kwanini tafiti ambazo zinafanyika katika vyuo vikuu vya Tanzania na matokeo yake yatatumiwa na Watanzania, taarifa zake nyingi hazipo kwenye lugha ya Kiswahili? Wakati umefika sasa kwa vyuo vya elimu ya juu kuwa na sera ya lugha itakayoruhusu wanafunzi kuandika taarifa zao za utafiti kwa Kiswahili au Kiingereza. Pia wakati umefika wa kuhakikisha kuwa tasnifu zote za shahada ya udaktari zinazoandikwa kwa Kiingereza zinakuwa na ufupisho kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika nchi ya Finland, tasnifu ambazo zitaandikwa kwa Kiingereza ni lazima ziwe na ufupisho au ikisiri kwa Kifinishi au Kiswidishi kutegemea aina ya chuo kikuu. Na kama lugha ya tasnifu ni Kifinishi au Kiswidishi lazima iwe na ufupisho au ikisiri kwa Kiingereza. Watanzania waliosoma nchini Finland tasnifu zao zina lugha mbili, na nyingine tatu kikiwemo Kiswahili.

Hoja ya Nne: Kwanini mafunzo ya theolojia katika ngazi ya shahada yanatolewa kwa Kiingereza wakati katika ngazi ya astashahada lugha ya Kiswahili inatumika? Maandiko mengi ya dini ya Kikristo yapo katika lugha ya Kiswahili na hata huduma nyingi za kiroho zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili. Pia tujiulize, kwanini programu za ngazi ya stashahada ambazo nyingi zinaandaa watendaji zinatumia Kiingereza kufundishia? Nionavyo mimi, wakati umefika sasa kwa vyuo vikuu kuanzisha programu ambazo Kiswahili kitatumika kama lugha ya kufundishia. Hili, litawawezesha wahitimu kujenga maana kwa kile walichojifunza kwa kuhusisha na muktadha halisi au maisha ya kila siku.

Hoja ya Tano: Kwa mujibu wa makala ya Aldin Mutembei, Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili ya chuo kikuu cha Dar es Salaaam iliandaa vitabu vya lugha ya Kiswahili kwa masomo ya sekondari ambavyo mpaka sasa havijatumika. Swali la kujiuliza, kwanini

---

[5] MoEST. (2017). National Strategy on Inclusive Education 2018-2021.
http://www.rodra.co.za/images/countries/tanzania/policies/National%20Strategy%20for%20Inclusive%20Education_version%20for%20signing.pdf

[6] Government of India. (2020). National Education Policy 2020. India: Ministry of Human Resource https://www.education.gov.in/sites/upload_files/mhrd/files/NEP_Final_English_0.pdf

[7] URT. (1995). *Education and training policy.* Dar es Salaam, Tanzania: Ministry of Education and Culture.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 9 06/07/2023 12:15 PM

Serikali isifanye majaribio ya kufundisha kwa kutumia Kiswahili katika shule chache za sekondari ili kuwa na taarifa za kisayansi zitakazosaidia kufanya maamuzi. Ikumbukwe kwamba elimu ni sayansi, kwa hiyo maamuzi yoyote lazima yafanywe kwa kuzingatia msingi ya kisayansi.

Hoja ya Sita: Kwanini wahitimu wa elimu ya sekondari na hata vyuo vikuu wana uwezo mdogo kwenye lugha ya Kiingereza wakati ndiyo lugha inayotumika kufundisha masomo yoyote? Hali hii, inamaanisha kuwa walimu wanaweka mkazo kwenye maudhui ya masomo kuliko lugha. Mwaka 2022 kwenye mjadala wa marekebisho ya Sera ya Elimu na Mitaala ilipendekezwa Kingereza kianze kufundishwa kuanzia elimu ya awali. Hata hivyo, hili sio pendekezo jipya, kwani kuanzia mwaka 2005 mpaka 2014 Kiingereza kilikuwa kinafundishwa kuanzia elimu ya awali na kabla ya 2005 kilikuwa kinaanza kufundishwa darasa la III na kurudishwa tena 2015. Swali la kujiuliza, Je sababu zilizoamua Kingereza kianze kufundisha darasa la III mwaka 2015 hazikuwa na mashiko au hazipo tena? Hakielimu (2021) inabainisha kuwa kujifunza lugha hakupewi kipaumbele cha kutosha kwenye elimu ya sekondari. Kwa mfano, hakuna mchepuo wa lugha ambao utatupatia walimu wenye umahiri wa kutosha. Na zaidi ya yote wanafunzi, wenye utendaji wa juu wengi wanashauriwa kujiunga na mchepuo wa sayansi.

Hitimisho

Mjadala wa matumizi ya lugha Kiswahili kufundishia katika ngazi zote za elimu bado unaendelea ukihusisha walimu, wanafunzi, watafiti, wazazi na watunga sera. Kwa ujumla kila matokeo ya mitihani ya kitaifa au upimaji yanapotolewa hoja ya lugha inajitokeza. Hoja zinazotolewa kwenye kitabu hiki zinalenga kuendeleza mjadala na kuthamini mchango wa wale ambao wameendelea kusisitiza manufaa ya kutumia Kiswahili kufundishia ikiwa ni pamoja na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Nategemea makala hizi chache zinaweza kujibu maswali ambayo tunajiuliza kuhusu hofu iliyopo katika kutekeleza jambo ambalo wapo watanzania wanaoliunga mkono.

MAREJELEO

Wizaya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WyEMU). (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo.* Dar es Salaam, Tanzania:

Brock-Utne, B. (2007). Language of instruction and student performance: New insights from research in Tanzania and South Africa. *International Review of Education,* 53, 509-30.

Government of India. (2020). *National Education Policy 2020.* India: Ministry of Human Resource https://www.education.gov.in/sites/upload_files/mhrd/files/NEP_Final_English_0.pdf

Osaki, K.M. (2001). Reflection on the change processes implied in the teacher education master plan in Tanzania. In G. Höjlund, N. Mtana & E. Mhando (Eds.), *Practice and possibility in teacher education in Africa: Perspective from Tanzania* (pp.58-70). Dar es Salaam: Ecoprint.

Msanjila, Y.P. (2010). Problems of teaching through the medium of Kiswahili in teacher training colleges in Tanzania. https://www.tandfonline.com/doi/pdf/10.1080/01434632.1990.9994419

Lewin, K.M., & Stuart, J.S. (2003). *Researching teacher education: Newperspective on practice, performance and policy.* Multi-Site teachereducation research project (MUSTER): Synthesis report. London: Department for International Development.

HakiElimu. (2021). *The Education We Want: A Critical Analysis of the Education and Training Policy (ETP) 2014, Issues, and Recommendations.* Dar es Salaam: HakiElimu

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 10 06/07/2023 12:15 PM

‘Gogo la Mti Lijapowekwa Mtoni Miaka 100 Haliwezi Kugeuka Mamba’ Tutumie Kiswahili kuwa Lugha ya Utambulisho na Kukuza Maarifa

Aldin K. Mutembei
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Utangulizi

Makala yangu ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza, ingawa itatanguliwa na maelezo ya kinadharia, inalenga kueleza hali iliyojengwa kuhusu Elimu. Makala itajaribu kuijengua hali hiyo kuhusu elimu. Sehemu ya pili nitajenga hoja kuhusiana na mnasaba uliopo baina ya Lugha na Elimu. Sehemu ya tatu, nitaeleza umuhimu wa kukitumia Kiswahili kuwa lugha ya kutolea na kuchochea maarifa. Sehemu ya nne na ya mwisho nitajaribu kupendekeza hatua za kuchukua ili Kiswahili kianze kutumika kufundishia.

Hoja zitakazotolewa katika sehemu zote nne zitaongozwa na nadharia ya Ubaadaukoloni (Ashcroft, 1995). Nadharia hii kama tutakavyoona, inaangalia taathira za ukoloni katika fikra na mienendo ya wale waliotawaliwa. Mjadala wetu utaangaliwa kupitia katika mada ya makala hili ambayo inachukuliwa kutoka msemo wa Kiafrika kuwa « Gogo la mti hata likiwekwa mtoni miaka 100, haliwezi kugeuka mamba » (Kenny, 2005 ; Mkondoni katika www.sampleposts.com). Kupitia katika msemo huu, makala itajadili jinsi fikra za baadhi ya Waafrika zinavyokengeushwa. Mkengeuko wa kitaasisi unaojengwa kutokana na kasumba ya ubora

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 11 06/07/2023 12:15 PM

wa wakoloni waliozitawala nchi za Kiafrika na udhaifu wa Waafrika waliotawaliwa. Kwa hakika ingawa swali lililoletwa katika Kongamano[8] lilikuwa « Ni kwa jinsi gani matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia shule za sekondari inavyoweza kuibua fikra tunduizi, uvumbuzi na utambulisho wa Mwafrika » ; na kujadiliwa kama mada au kama waandaaji walivyoandika: "How can the use of Kiswahili as a language of instruction in secondary schools enhance critical thinking, innovation and African identity", kutokana na hali halisi ; kwa hakika mada kuu ingetakiwa kuwa "ulazima na uharaka wa kukitumia Kiswahili katika kukuza ujifunzaji na upimaji maarifa, kuibua frikra tunduizi na kujenga utambulisho wa Mwafrika". Aidha, Kiswahili hapa kinatumika tu ili kuujadili muktadha wa Tanzania (na labda mahali kwingine kokote kinapotumika Kiswahili). Vinginevyo, lugha za Kiafrika hazina budi kujisimamia katika ukuzaji maarifa kwa jamii zao bila ya kuegemea katika lugha za kikoloni za Kifaransa, Kiingereza au Kireno (kutegemea ni jamii ipi ilitawaliwa na mkoloni yupi). Utangulizi huu, unatuingiza katika sehemu kuu ya mjadala wetu, ambao utatanguliwa na maelezo ya kinadharia yafuatayo :

Sehemu ya Kwanza : Utangulizi wa Kinadharia

Mawazo ya Edward Said (1995), ambayo hapa tunayachukua kama msingi wa nadharia ya Ubaadaukoloni, anayafafanua kupitia dhana yake ya "Orientalism" (Umashariki). Hii ni dhana ya kidhahania ambapo watu wa Magharibi (wakoloni) kijamii, walimuumba, kumwelekeza na hasa kifikra; kumtawala huku kimwili wakimkandamiza mtu (au jamii) mtawaliwa katika eneo dhahania la mashariki (Said, 1995 : 88-89). Katika kumuumba huku, mtu aliyetawaliwa hujikuta kifikra, kimwonekano, na kitabia akijitahidi kuwa kama « muumbaji » wake, mkoloni. Nadharia ya Ubaadaukoloni kwa kuhusiana na lugha imeelezwa na Frantz Fanon (2008) akianza na swali hili : Je yawezekana(je) mtu mweusi akaendelea na kueleza utu wake kwa kutumia lugha, vifaa na nyenzo za ustaarabu wa kimagharibi (2008 : vx) ? Swali hili ni muhimu katika makala yetu kwa kuwa, linauangalia kwa unyume msemo unaobeba kichwa cha makala hii. Fanon (2008) anaendelea kusema kuwa, kuongea ni kuonesha ulimwengu unaosikiliza kuwa mwongeaji yupo, anaishi na anawakilisha kuwapo kwake. Hata hivyo, kwa Waafrika waliokumbatia lugha za wakoloni, Fanon anaeleza kuwa kuongea kwao huwa wanajitahidi kujionesha kwa mtawala wao (ambaye wanaongea lugha yake), kuwa wapo na wanajitahidi kufanana na yeye (2008 :8). Kwa muktadha wa kichwa cha makala hii, huko ni kujitahidi kuwa mamba, hata pale inapojulikana kuwa hilo ni gogo la mti lililowekwa ndani ya maji. Hata hivyo, Fanon anatukumbusha kuwa, kuongea, sio tu kufahamu sintaksia na mofolojia ya lugha, bali unapoongea, unauonesha utamaduni, unaubeba ustaarabu unaowakilishwa na lugha husika.

Mzungumzaji anapotumia lugha yake ya asili, huonesha kuwa anaumiliki ulimwengu ambao unaumbwa na kuelezwa kupitia katika lugha hiyo. Kwa hiyo, mtu anapozungumza kupitia katika lugha isiyo ya kwake, humaanisha pia kuwa anauona ulimwengu kupitia kwa jinsi unavyoonwa na wenye lugha hiyo. Hii maana yake ni kuwa, wale waongeao lugha ambazo si za asili yao, hawawezi kuwa na ulimwengu halisi. Kwao, ulimwengu huwa kivuli cha ulimwengu halisi. Ukweli huo huwa mbaya zaidi na wenye athari hasi ikiwa lugha hizo hupitishwa kama lugha za elimu na zikatumika kutolea maarifa. Kamwe wanaopewa elimu hiyo, hawawezi kupata maarifa inavyotarajiwa. Na kwa mujibu wa makala hii, ni kujaribu kuyageuza magogo kuwa mamba, kwakuwa tu, yamo ndani ya maji.

Mwafrika anapoongea Kiingereza, Kifaransa au Kireno, anasema Fanon (2008), hujiona kama amepandishwa hadhi, kama ambaye amenyanyuliwa kutoka mwituni, akijilinganisha na ustaarabu na hadhi inayobebwa na mila na tamaduni zake kupitia katika lugha yake ya asili (2008 :9). Mawazo haya ni ya hatari sana katika mustakabali wa maendeleo na utambulisho wa Waafrika. Ni mawazo ya hatari yanayoingizwa kama sumu kupitia katika mfumo wa elimu unaolazimisha wanafunzi kufundishwa kupitia katika lugha isiyokuwa ya asili wala yenye uhusiano na mila na tamaduni zinazowazunguka. Katika baadhi ya shule mawazo haya ya hatari huanzishwa kwa desturi za adhabu kama kumvalisha gunia au kumvalisha kibao kilichoandikwa maneno ya dharau au ya kudhalilisha baada ya mwanafunzi kuongea lugha ya Kiswahili (Tibategeza, 2010 ; 2018). Mwanafunzi anayevalishwa kigunia au kibao huchekwa na wenzake. Huingia katika mtanziko wa kisaikolojia kwa maana ingawa kifikra hujiona hana hatia kwa kuongea lugha yake, katika hali ya kushangaza shule yake humpa adhabu. Itakumbukwa kuwa mwanafunzi anapoingia shuleni kwa mara ya kwanza, anakuwa na matumaini makubwa na maono kama inavyotarajiwa kutoka mtu mwenye hamu ya kupata maarifa. Sehemu ifuatayo inajadili hali hii.

[8] Makala hii inatokana na wasilisho lililotolewa katika Kongamano lililoandaliwa na Kigoda cha Mwalimu na kuratibiwa na Haki Elimu na kufanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 10 Juni, 2022.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 12 06/07/2023 12:15 PM

Ndoto za mwanafunzi shuleni

Katika shule nyingi za msingi nchini Tanzania kuna kauli mbiu isemayo : Elimu ni Ufunguo wa Maisha (Twaweza, 2015). Kauli hii ni matarajio ya wanafunzi, walimu na wazazi au walezi. Zamani wakati wazazi na walezi wengi walikuwa na mali ya kurithisha kama mashamba na mifugo, ilikuwa ni matarajio yao kuwa wanafunzi wakipatiwa ufunguo wa elimu ya maisha wataweza kujimudu na kuinua urithi wao kwa ajili ya maendeleo yao na jamii zao. Uwezo kama huo si mwingi kwa wazazi na walezi wa sasa. Wengi wana fedha kidogo (kama ipo) ambayo wanajinyima na kuwekeza katika elimu ya watoto, wakitarajia kuwa maisha mazuri yatafunguka mbele yao na kwa mustakabali wa jamii pana na utangamano wa taifa. Kwa hiyo wanapowapeleka shule za msingi na kukuta kauli mbiu kama hiyo : Elimu ni ufunguo wa maisha (Mihyo, na wenzake, 2021), wanarejea nyumbani wakiamini kuwa maisha ya watoto wao yatafunguliwa kwa elimu watakayoipata. Hata hivyo, baada ya muda mrefu wa kuona kuwa hakuna maisha yanayofunguka, wazazi na walezi wengi baadayea hujiuliza : Unafungua kuingia katika maisha gani ?

Inaposemwa dhana ya 'kufungua', tujue ipo pia dhana ya 'kufunga'. Kwahiyo, ni lazima kujiuliza, tena kwa uchunguzi wa dhati kabisa : Wanafunzi wamejifungia wapi ? Ni nini kilichowafunga ? Na sasa, wanafunguliwa kuingia maisha yepi ? Maswali haya yanaonesha tatizo pana katika mfumo wa elimu (Mlama na Matteru, 1978 ; Campbell, na Qorro, 1997). Walimu waliofundishwa kupitia lugha isiyo ya asili kwao, wanaufahamu ambao ni wa mashaka. Yale wanayodhani wanayajua ili yawe kichocheo katika kufundisha watoto, nayo ni mashaka makubwa. Na kile wanachokieleza kwa wanafunzi hakina msingi utarajiwao.

Baada ya miaka saba ya kujaribu kujenga msingi na matumaini ya kufungua maisha kupitia katika elimu (Gaddis na Hoogeveen, 2015), ghafla wanafunzi wanaotumaini kuendelea, hujikuta kwenye lango kubwa linalojifunga taratibu mbele yao. Jitihada zilizofanywa kufungua milango mbalimbali ya udadisi, ufumbuzi na upatikanaji maarifa mbalimbali katika shule ya msingi (NUFFIC, 2014 ; Gaddis na Hoogeveen, 2015), hujikuta zinaangaliana na ukuta ambao huondoa taratibu matumaini ya kuendelea kujengwa kwa udadisi, uchunguzi, ugunduzi, ufumbuzi na upatikanaji maarifa. Matumaini ya kufunguka kwa maisha bora kwa wanafunzi na wazazi wao huishia hapo (Rubagumya, 1997 ; Rugatiri, 1997 ; Mtallo, 2015). Muda na nguvu za walimu waliowekeza katika ufundishaji shule za msingi husutwa na mbwembwe za Kiingereza; huku matarajio ya jamii pana ya taifa la Tanzania yakiwa yananing'inia (Criper, na Dodd, 1984). Hapa ndipo huwa mwanzo wa maangamizi ya elimu (Senkoro, 2007).

Mbele ya halaiki ya watoto hawa, ghafla elimu inakoma kuwa ufunguo, inabakia ni pambo. Pambo linaloendelea kumsuta mzazi aliyewekeza katika elimu, na kumuumiza mwanafunzi katika maisha yake yote yaliyoko mbele yake.

Ingawa kutokea miaka ya sitini (1960) tafiti nyingi na zote za kisayansi zimehitimisha kuwa lugha inayotakiwa kuwapatia maarifa na hivyo kupata maendeleo ya kweli kwa Watanzania na kukuza uwezo wa fikra tunduizi, uwezo wa sayansi na ugunduzi; ni Kiswahili (Kiimbila, 1971; Mlama na Matteru, 1978; Criper, na Dodd, 1984; Brock-Utne, 1993: Rubagumya, 1997; Campbell, na Qorro, 1997 ; HakiElimu, 2017-2021 ;-); Shirika lisilo la Kiserikali, Hakielimu limekuwa likitetea waziwazi tokea mwaka 2001 kuwa, ni haki mwanafunzi apewe elimu katika lugha ya Kiswahili (Carlitz, 2013). Ukweli huu umekuwa ukisalitiwa na umezungukwa na unafiki na ulaghai katika sura zake mbalimbali hata umeshindwa kutekelezeka hadi leo. Mahali pengine, hali hii imeitwa 'laana' (Mtallo, 2015); au imeonekana kuwa ni marejeo ya ukoloni katika fikra za Mwafrika (Brock-Utne, 2000). Fikra hizi za utegemezi katika lugha ni moja ya mambo yaliyopingwa katika Elimu ya Kujitegemea.

Mawazo ya Mwalimu Nyerere kuhusu Elimu ya Kujitegemea, yalichapishwa kwa mara ya kwanza kama Sera, Machi 1967. Katika utangulizi wa Sera hiyo, Mwalimu anasema: Only when we are clear about the kind of society we are trying to build can we design our educational service to serve our goals. Mpaka pale tutakapojua waziwazi ni jamii ipi tunayotaka kuijenga, ndipo tutakapoweza kuandaa mitaala ya elimu itakayoweza kutimiza malengo yetu (1967:1). Malengo ya Elimu ya Kujitegemea yaliweka wazi maana ya kujitegemea. Mwalimu alihusisha lugha iliyokaribu na watu, ambayo watu wanaitumia kila siku, na Elimu ambayo nchi ilikuwa inaitarajia kwa maendeleo ya wale waipatayo na kwa faida ya taifa kwa ujumla. Lugha ya Kiswahili ilikidhi malengo ya Elimu ya Kujitegemea hivyo ikawa rasmi lugha ya kutolea elimu ya kujitegemea na kujenga maarifa katika shule za msingi kuanzia mwaka 1968 katika kutekeleza sera hii. Lakini sera hii ilisalitiwa (Brock-Utne, 1993). Leo kuna shule za msingi hasa za binafsi zinazoendeshwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Watoto wanaosoma katika shule hizi, wanatokea katika mazingira na utamaduni wa Uswahilini, na huko ndiko wanakorejea kila wakati wa likizo. Wafanyabiashara wenye shule hizi ni kama wanawaona watoto hawa kama magogo yaliyowekwa ndani ya maji, wakiwaaminisha

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 13 06/07/2023 12:15 PM

wazazi na walezi wao kuwa siku moja watabadilika kuwa mamba. Watakuwa Waingereza, kwa kuwa wamezoea Kiingereza. Hata hivyo, mazingira yanayowazunguka watoto wa shule hizi za msingi, tamaduni na desturi ni zile za Uswahilini, ambako Kiingereza ni nadra kukutwa kikitumiwa kama lugha ya kawaida katika maisha yao.

Mjadala wa sera hii na hasa kuhusiana na lugha ya Kiswahili kuwa ya kufundishia ulikuwa mkubwa kiasi kwamba, mwaka 1971, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichapisha kitabu kilichoitwa Kichocheo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Katika kitabu hicho sura ya kumi inaongelea "Matumizi ya Kiswahili nchini, shuleni na Vyuoni" (Kiimbila, 1971: 60 – 72). Kiimbila anaonesha hoja 15 zilizotolewa na wale waliopinga matumizi ya lugha ya Kiswahili wakati huo mwaka 1971. Anaonesha hoja zao; na anaweka bayana majibu ya hoja hizo huku akionesha udhaifu wa kila hoja iliyotolewa. Anasisitiza kuwa uchaguzi wa kukitumia Kiswahili ulikuwa ni uamuzi bora kabisa.

Kwa faida ya msomaji wa makala hii, hoja hizo 15 za mwaka 1971 ndiyo hoja hizo hizo zinazotolewa na wanaopinga matumizi ya Kiswahili leo mwaka 2023. Kwa maneno mengine, hoja za kukipinga Kiswahili zilizojengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, ndiyo hizo hizo zinazotumika leo, bila ya kujua au kujali kuwa lugha ya Kiswahili imepiga hatua kubwa sana, imeendelea kimsamiati na kimatumizi, imeenea na inasomwa vyuoni na katika sehemu na nyanja mbalimbali duniani.
Mojawapo ya sababu ambayo inashikiliwa na wanaopinga ni kuwa mtu akifundishwa kwa Kiswahili hawezi kuwasiliana na watu wengine nje ya Tanzania, na maisha yake yatabaki kuwa ni ya humu humu Tanzania (kama kwamba hiyo ni dhambi kubwa). Tanzania ambayo elimu yake itatolewa kwa kutumia Kiswahili, wanadai, itakuwa kisiwa (Mwassa, katika The Citizen). Niruhusuni hapa nikupe mifano michache inayopinga mawazo haya.

Katika nchi zinazotumia lugha zao kufundishia na kutolea maarifa, wananchi wake wameng'ara na kupata tuzo za dunia katika sekta mbalimbali. Uarabuni, kwa mfano, Ahmed Zewail alisoma masomo yake yote ya shahada ya kwanza 'BSc' na ya pili 'MSc' kwa Kiarabu. Alikuwa akijifunza Kiingereza kama somo. Alikwenda kusoma PhD nje ya Uarabuni. Kutokana na kuwa na maarifa na kujengewa hali ya udadisi alipata Tuzo ya Nobel katika Kemia mwaka 1999. Anayaeleza haya katika kitabu chake kiitwacho: "Voyage Through Time: Walks of Life to the Nobel Prize" kilichochapishwa mwaka 2004.

Nchini China, kuna zaidi ya Wachina 20 ambao wamepata Tuzo za Nobel katika Nyanja za Fizikia, Kemia, Fiziolojia, Fasihi, na Utabibu (Medicine). Wote hao walipata elimu zao kupitia Lugha ya Kichina, hali wakijifunza Kiingereza kama somo. Leo dunia nzima inawatambua. Kwa hiyo, sababu hiyo inayotolewa haina msingi wowote, ni ulaghai, unafiki na usaliti. Lugha ni uchumi. Na wengi wanaopinga wanaujenga na kuuimarisha uchumi wa Waingereza kupitia katika Kiingereza kwa kukipinga Kiswahili; ni unafiki na usaliti. Niruhusuni sasa kueleza kwa kifupi ninamaanisha nini ninaposema kuhusu unafiki na usaliti.

Kiwango na Hatari Iliyopo

Juzi (Mei 2022) nilikuwa nasikiliza kuhusu mauaji ya watoto na walimu wasio na hatia katika jiji la Texas nchini Marekani (AP News). Nikasikitika sana na kuziombea roho za marehemu pumziko la milele. Mauaji mabaya sana. Lakini yafaa nini kuzungumzia mauaji hayo; utolewaji wa roho zisizo na hatia Marekani, ilihali hapa hapa Tanzania kuna mauaji ya maarifa na matarajio ya wanafunzi wengi yanayofanywa na mfumo wa elimu kwa mamilioni ya watoto wasio na hatia (Senkoro, 2007; Weston, 2016; Kevogo, 2018). Ninazungumzia kiwango cha unafiki ambacho Weston anaieleza hali hiyo ya utolewaji elimu kuwa ni kujeruhi hadi kutokeza ulemavu wa kushindwa kutembea (Weston, 2016).

Tena, nikasikiliza katika vyombo vya habari kuhusu kilio cha kuzagaa bunduki mitaani kisheria, (Scudder, 2022; Cai, 2022) ambazo zimekuwa zikitumika kuwaua watoto (Cai, 2022; Spagat na Coronado, 2022). Watoto na vijana wengi wasio na hatia katika Majiji na Vitongoji vya majimbo ya Marekani.

Kinachonifikirisha katika taarifa hizo kutoka vyombo mbalimbali ni jinsi ambavyo, Watoto wanalalamika; walimu wao wanalalamika. Wazazi wanalalamika kuwa Watoto wao wanauawa bila hatia; Polisi nao wanalalamika. Kabla sijashangaa sana, nikasikia na Wabunge wanalalamika. Watunga sheria wanalalamika na hata nikawasikia viongozi waandamizi wa serikali mbalimbali wanalalamika (npr.org, 2022). Nilishangaa zaidi kumsikia hata mheshimiwa raisi wa Marekani analalamika (www.whitehouse.gov). Nilianza kufikiri kutokea wakati huo, na ninaendelea kufikiri kuhusu dunia na maamuzi yake. Lakini yanini

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 14 06/07/2023 12:15 PM

kukaa nikishangaa na kufikiria kuhusiana na mauaji ya kila mara ya Watoto hao yanayofanywa na bunduki zilizotapakaa kisheria mikononi mwa wananchi. Kumbuka bunduki hizo zinatapakaa kisheria. Ya nini hayo, ilihali mauaji ya maarifa yanafanywa katika nchi nyingi za Kiafrika kupitia katika bunduki ya Elimu. Ki-miongozo na kisheria. Hakuna uuaji mbaya kama ule unaofanya kupitia elimu. Uwezo wa Maarifa kwa vijana wetu unauawa kupitia katika bunduki ya elimu. Kinachoshangaza.
Kinachoshangaza, wanafunzi wanalalamika, walimu wao wanalalamika, wazazi wanalalamika (dar24.com) kuwa ni Elimu imefanywa isiwe Ufunguo wa Maisha. Wabunge watunga sheria nao wanalalamika (The Citizen, 2019). Viongozi waandamizi wa serikali wanalalamika (Tamisemi.go.tz). Kwa maneno mengine anayepewa elimu analalamika, na anayetoa elimu naye analalamika. Kiwango cha malalamiko kimeendana na kiwango cha kukua kwa unafiki kutokea mwanzoni mwa miaka ya sabini. Hiki ni kiwango cha ajabu cha unafiki ambapo Barrett (1994) anaonesha kuwa kikwazo kimekuwa utashi wa kisiasa, kwa maana wanasiasa wanafaidika na kuwapo kwa matumizi ya Kiingereza, (Rubagumya, 2010) kwa gharama ya kutokuwapatia wajifunzaji maarifa au thamani ya elimu waitarajiayo. Viwango vyote vya unafiki vimeendana na kukua kwa kiwango cha usaliti. Ambacho sasa ninapendekeza tukiangalie kwa umakini.

Kutoka Unafiki hadi Usaliti

Na wote ni Watanzania, na wote tunajenga Tanzania yetu moja, na wote, ninadhani tunajivuna kuwa Watanzania. Lakini kuna wale ambao ujenzi wao kwa Tanzania unashangaza. Kuna wale wanaodai kuwa, kutumia Kiingereza kufundishia ni kuwafungulia maisha wanafunzi maana wataweza kuwasiliana na wenzao nje ya Tanzania, na Tanzania haitakuwa kisiwa (Mufuruki, 2015; Kanyabwoya, 2021; Mosenda, 2022). Kwa maneno mengine, kama wangelifanikiwa, wangewafanya Watanzania wanaopata elimu hiyo ya Kiingereza kwenda nje ya Tanzania ili wakiwa na maisha mazuri huko nje, watatokea huko kuiendeleza Tanzania. Na mawazo haya yanatolewa na wasomi na wanazuoni. Mantiki yao ni ya ajabu, kwamba wasomi wenye Kiingereza wataijenga Tanzania kwa kutokea nje ya Tanzania. Au kama wao wasemavyo, by remote control. Lakini hata kama hoja yao ingeweza kuwa na mantiki, wanachanganya jambo moja kubwa: mtu hajifunzi lugha ngeni kutokana na kuwa lugha hiyo inatumika kufundishia. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa mtu hujifunza lugha ngeni ikiwa lugha hiyo itafundishwa kama somo na walimu waliomahiri (Qorro, 2013).

Matumizi ya lugha isiyokuwa na mizizi katika maisha ya kawaida ya Watanzania, imeifanya elimu kuwa pambo badala ya kuwa ufunguo. Na wanaoshikilia kuwa tuendelee kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia hawajali kuwa mjifunzaji anapata maarifa ama hapati. Akiweza kuongea Kiingereza, kwao ni alama ya kusoma, ni alama ya elimu. Au kwa maneno mengine, kule ambako hakuna Kiingereza, Japan, Ujerumani, Korea, nchi za Skandinavia n.k.; hawajasoma, hakuna elimu. Kwa watetezi wa Kiingereza Tanzania, mwanafunzi akiisha kukariri, kwao inatosha kuonesha kuwa amesoma, kuwa ana elimu. Kinachowahusu watetezi wa Kiingereza kama lugha ya kufundishia, ni kujaribu kuwafanya watoto wa Kitanzania kuwa watoto wa Kiingereza. Jitihada hii inafanywa, huku ikitetewa na baadhi ya wasomi kuona kuwa gogo la mti waliloliweka ndani ya maji siku moja litageuka kuwa mamba. Mamba wa Kiingereza.

Baadhi ya wenye elimu hawaisaidii jamii iliyowapa elimu ili ijikwamue kutokana na changamoto zilizopo. Hawa ni wasaliti. Mwalimu Nyerere aliwaonya watu kama hao kupitia katika hotuba yake katika mahafali ya Wanachuo, na nukuu yake inaweza kuonekana kwenye ukuta nje ya ukuta wa ukumbi wa maktaba ya Chuo Kikuu cha dar es Salaam. Mwalimu Nyerere akiwa Mkuu wa Chuo Kikuu wakati huo alikuwa akiwaasa wanachuo kuwa hawana budi kurejea vijijini katika jamii zao ili waitumie elimu waliyoipata kuzikomboza jamii hizo. Wasiporejea, alisema ni usaliti. Huo ndiyo usaliti, lakini kwa mkuktadha wa mjadala huu, zaidi ni unafiki; kwakuwa inatarajiwa kuwa msomi anajua uhusiano baina ya Lugha na Elimu, au tusema Lugha na ujenzi wa maarifa. Anatarajiwa kujua kuwa ufundishaji wa lugha ya kigeni kama somo, na lugha inayotumika kufundishia kuwa ni mambo mawili tofauti. Ikiwa hajui, kuna tatizo katika kusoma kwake. Niruhusuni japo kwa kifupi kuonesha uhusiano uliopo baina ya elimu na lugha.

Sehemu ya Pili: Mnasaba kati ya Lugha na Elimu

Upo mnasaba mkubwa baina ya Lugha na Elimu. Lugha ambao ni mfumo wa mawasiliano unaohusisha maneno na kanuni, hudaka kwa haraka yale yasemwayo na kuyachakata ili kuyapa maana ikiwa yasemwayo yanatokea katika mazingira yaliyozoeleka.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 15 06/07/2023 12:15 PM

Mawazo yanayoweza kueleza mnasaba huu ni yale yaliyotolewa na David Klaus (2001) aliposema "Kwa ujumla kuna kukubaliana kuwa wanafunzi hujifunza vizuri zaidi wanapokuwa wanaelewa mwalimu anachosema". Ikiwa mwanafunzi haelewi vizuri mwalimu kasema nini, ni vigumu kuchakata kilichosemwa na hivyo ni vigumu kabisa kupata maana. Ukweli wa alichokisema Klaus ulisisitizwa na Mekacha (1997) alipoangalia ubora wa elimu inayotolewa. Mekacha alisema, lugha ndiyo huamua ubora wa elimu inayotolewa. Ikiwa lugha inaeleweka, imo katika matumizi ya kawaida, na wanafunzi huitumia lugha hiyo katika maisha yao ya kila siku; basi lugha hiyo ikitumika kutolea maarifa, ni dhahiri kuwa mjifunzaji atapata elimu bora (1997). Halima Mohammed Mwinsheikhe, (2001) alipiga hatua zaidi na kuonesha kuwa si elimu kwa ujumla tu inayoimarishwa kutokana na lugha inayofahamika; bali katika utafiti wake anaonesha kuwa katika masomo ya sayansi wanafunzi wanakumbana na kizingiti wanaposomeshwa katika lugha wasiyoifahamu. Kuwa, uelewa na uchakataji wa maarifa wanayoyapata haufanyiki inavyotarajiwa katika masomo ya sayansi pale wanafunzi wanapofundishwa katika lugha ngeni. Anaonesha kuwa ikiwa mfumo utabadilika, na Kiswahili kikatumika kufundishia masomo ya sayansi, kizingiti kitaondoka, na wanafunzi walio wengi wataweza kupata maarifa, kuyachakata, kujenga udadisi na hatimaye kuwa wanayasansi mahiri. Katika hali hii, isichukuliwe kuwa mtu ajifunzaye hana ajuacho. Yupo tu pale kupokea yasemwayo kutoka kwa mtu anajeyua, yaani Mwalimu. Ni muhimu kujua kuwa, elimu katika lugha sahihi, humsaidia mwanafunzi kuzindua yale ambayo ubongo wake huyabaini. Humfanya mwanafunzi aanze kuwa na fikra za kujitegemea. Kutafuta mwenyewe maarifa, kujazia na kuendeleza yale yaliyotolewa kama kichocheo darasani. Katika kila ngazi mahususi ya maarifa, mwanafunzi huwa na ujuzi na stadi ambazo zimejengwa na kuchochewa na matumizi ya lugha anayoifahamu. Hayo ndiyo yaliyomo katika falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, kama ilivyojifafanua katika sera hiyo ya Mwalimu ya mwaka 1967.

Mawazo ya Mwalimu Nyerere kaitika Elimu ya Kujitegemea, yanakaribiana na yale ya Paulo Freire (1968) alipoielezea dhana ya Elimu benki (Banking education). Kuwa mwanafunzi asifanywe kupokea tu maarifa, bali awezeshwe kuanzisha fikra zake mwenyewe ambazo zitamfanya kumudu maisha yake bila kutegemea msaada. Isiwe mwalimu anaonekana ndiye mwenye maarifa anampatia mwanafunzi, kama mteja awekavyo fedha zake benki, na mwanafunzi ni wa kupokea tu. Jambo hili linatuingiza katika ujenzi wa fikra tunduizi unavyowezeshwa na lugha inayofahamika.

Lugha na Fikra Tunduizi

Kuna uhusiano mkubwa baina ya lugha aijuayo mtu na kukua kwa fikra tunduizi. Kwa hakika yote mawili hukua pamoja, moja likiliendeleza jingine (Nikoopour na wenzake, 2011; Bagheri, 2015). Vipo vipengele takriban nane vinavyoonesha uhusiano chanya baina ya lugha inayofahamika na ufahamu wa mtu anayeitumia lugha hiyo. Vipengele hivyo kwa pamoja ndivyo hujenga hali ya utunduizi katika mawazo na fikra za mtu. Hali hiyo kwa mtu hukuza na kuendeleza udadisi, ugunduzi na hata ufumbuzi wa mambo. Tuviangalie vipengele hivyo kwa kifupi tu: Mtu akiwa na lugha anayoifahamu, basi lugha humjengea kujiamini (Tunçel, 2015). Lugha inayofahamika humwondolea mwenye kuijua woga. Humpa ujasiri wa kutumia msamiati mahali sahihi (Fanon, 2008: 8-9), na kwa maana anayoikusudia:

- Lugha inayofahamika humfanya mwenye kuitumia kukuza uwezo wake wa kujieleza.
- Lugha inayofahamika humfanya mwenye kuitumia kukuza uwezo wake wa kutathmini mambo.
- Lugha inayofahamika humfanya mwenye kuitumia kukuza uwezo wake wa kufikiri jambo linaloweza kutokea ikiwa uamuzi fulani utafanyika au kinyume chake.
- Lugha inayofahamika humfanya mwenye kuitumia kukuza uwezo wake wa kufahamu tatizo (Pickering, na Gambi, 2018) au kufahamu changamoto zilizopo na kuweza kuzitatua.
- Lugha inayofahamika humfanya mwenye kuitumia kukuza uwezo wake wa kujenga hoja (Brock-Utne, 2007; Hinton, 2019), na kuitetea.

Vipengele hivi vyote kwa pamoja humfanya mwenye navyo kuwa na fikra tunduizi. Kadri mtu anavyoendeleza fikra tunduizi, ndivyo umilisi wake wa lugha unavyoongezeka. Na jinsi ujuzi na umilisi wa lugha unavyokua, ndivyo uwezo wa fikra tunduizi za mtu unavyoongezeka. Kuongezeka huko huinua kiwango cha ubunifu; na ikiwa mtu huyo anaegemea katika masomo ya sayansi tumizi, ndivyo pia udadisi wake unavyokua na kuchochea hali ya uchunguzi na upatikanaji wa maarifa. Katika kiwango cha juu cha hali hii, ndipo tunapopata ugunduzi wa mambo, na ufumbuzi wa tatizo lililokuwapo katika jamii.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 16 06/07/2023 12:15 PM

Mambo haya hayawezi kufanikiwa kwa kutumia lugha isiyofahamika. Wanafunzi wanaofundishwa kupitia lugha ngeni wasidhaniwe tu kuwa ghafla watakuwa na maarifa na fikra tunduizi. Wachache wanaobahatika kuwa na hali hiyo, ni jitihada na kipaji binafsi na ni baada ya kusumbuka sana. Ndiyo maana ni muhimu sana, na hapa nafanya kusisitiza tu, kwani ukweli huu umesemwa mahali pengi na wataalamu wanazuoni wenye maono, kuwa kuna ulazima wa kutumia lugha inayoeleweka katika kutolea elimu na kujenga maarifa ikiwa taifa linataka kuendelea. Na kwa hapa Tanzania, lugha hiyo ni Kiswahili. Sehemu ifuatayo itatoa hoja kuueleza ukweli huo.

Sehemu ya Tatu: Kiswahili Lugha ya Kutolea na Kuchochea Maarifa

Leo, mwaka 2022 sio mwaka 1971. Kama ilivyooneshwa awali, mjadala wa lugha ya kufundishia ulifanyika kwa kina mwaka 1971 hata kukatokea chapisho lililoitwa Kichocheo cha Lugha ya Kiswahili (Kiimbila, 1971). Lakini leo hii ukiacha mjadala kama huo, walimu waliowengi tayari wanatumia Kiswahili kufundishia sekondari hata vyuoni (Roy-Campbell na Qorro, 1997). Huu ni ukweli ambao pengine katika vikao rasmi haidhaniwi kuwa utaongelewa.

Leo hii, wanafunzi wengi wanajadili masomo ambayo si ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili (Lupogo, 2014). Katika shule za sekondari na hata katika vyuo si jambo la ajabu kukuta mjadala wa Kemia, Biolojia, Hisabati, Jiografia au Historia ukifanywa kwa Kiswahili tena wanafunzi wakijiamini kabisa. Huo ndiyo ukweli, kinachobaki sasa ni kuifanya rasmi matumizi ya Kiswahili.

Kama Tanzania ingeanza kutumia Kiswahili wakati huo, mwaka 1971, leo nchi hii ingekuwa mbali katika maendeleo na uchumi wake ungekuwa wa kiwango cha juu. Mapinduzi katika uamuzi wa kutumia lugha inayofahamika zaidi na watu katika kutolea maarifa ndiyo uliozibadilisha nchi kama Uingereza, Finiland, na hivi karibuni Malaysia, Indonesia na Korea kwa kutaja tu kwa uchache. Nchi nyingine zote zilizoendelea duniani zilitumia lugha zao wenyewe kuinuka na kuwa na maendeleo.

Malaysia ambayo ilikuwa fukara hadi katikati ya miaka ya 60, kama Tanzania; baada ya mwaka 1990 ilianza kukua kiuchumi na kuonesha maajabu duniani. Leo tunapokwenda kwao kujifunza walifanya maajabu gani, na kuanza msamiati wa "matokeo makubwa sasa" (Janus & Keijzer, 2015), tunadharau kuwa moja ya nguzo katika kuwezesha maajabu yao ilikuwa mabadiliko katika lugha ya kujifunzia. Malaysia ambayo ilikuwa ikitumia Kiingereza na Kitamil ilibadili mwelekeo na tangu 1967 ikaanza kutumia KiMalay (Azmi, 2013). Shule zote zilizokuwa za mchepuo wa Kiingereza zilibadilishwa na kuanza kutumia Kimalay. Mabadiliko hayo yalifanyika kwa awamu. Azmi anazema "...kwa kuanza kukitumia Kimalay kama lugha pekee ya ufundishaji katika shule za taifa, Kiingereza kilibaki kufundishwa kama somo (2013:2). Na hata baada ya kurudia uamuzi wa kukitumia Kiingereza kuwa lugha ya kufundishia mwaka 2003, baadaye Bunge liliamua kuwa masomo ya sayansi na hisabati yarejeshwe kufundishwa kwa Kimalay, mwaka 2009. (2013:3). Labda ukweli huu, ndiyo uliosababisha Tanzania ikubali kwa mara ya kwanza kupitia sera ya Taifa ya Elimu ya 2014 kuwa Kiswahili kifanywe kuwa Lugha ya kutolea elimu katika ngazi zote za elimu (Taz Sera ya Elimu 2014. Kifungu 3.2.19, ukurasa 38).

Pamoja na kuchelewa kwa miaka zaidi ya 50, hatimaye sasa Sera ya Elimu (2014) imeruhusu. Hii inatukumbusha historia ya Waingereza waliokuwa wanaidharau lugha yao wenyewe na kuiona kuwa ya kishezi baada ya kuwa wametawaliwa na Warumi kwa zaidi ya miaka mia tatu (Vance, 2000). Iliwachukua muda kukithamini Kiingereza na kuanza kukitumia, lakini leo hii huo uliokuwa unaitwa ushenzi wa Kiingereza tunaona hadhi yake.

Kiswahili leo ni lugha inaenea kwa kasi sana. Haibaki kuwa ni lugha ya Upwa wa Afrika Mashariki, bali sasa inaelekea kuwa Lugha ya Mawasiliano mapana katika Afrika nzima. Imekuwa lugha rasmi katika nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki. Imekubaliwa kuwa lugha rasmi katika Ukanda wa Maendeleo Kusini mwa Afrika SADC, na imekubaliwa kuwa lugha rasmi na lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika – AU. Kwa kifupi, ingawa Kiswahili kinakuwa kwa kasi, na kuuelekea Uafrika, ni muhimu kujikumbusha nafasi yake katika Tanzania.

Tanzania ni nchi ya Kiswahili. Kiswahili sanifu kinachofundishwa kama lugha rasmi dunia nzima kinaegemea katika lahaja ya Unguja, Tanzania. Ni muhimu Tanzania itangulie kuonesha njia ya namna ya kupata elimu bora kwa kuifanya lugha ya kujifunzia na kufundishia na kukuza maarifa kwa Kiswahili.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 17 06/07/2023 12:15 PM

Kuanzia katika mafunzo ya sayansi kwa shule za msingi, walimu wabobevu wameandika vitabu vya sayansi kwa kutumia mtaala wa sekondari. Hivyo, leo ikiamuliwa kuanza kutumia Kiswahili kufundishia, tayari kuna vitabu vya kuanzia kwa Kidato cha kwanza na cha pili. Upo msamiati wa teknolojia na unaongezeka kadri teknolojia inavyobadilika kama zifanyavyo lugha nyingine zote duniani. Upo msamiati na kamusi ya Utabibu. Msamiati huo unaendelea kukua kwa kadri weledi wa Nyanja hozi unavyozidi kukua. Upo msamiati mwingi katika nyanja mbalimbali unaosubiri kuingia katika matumizi rasmi.

Lakini pia, na hii ni muhimu sana, Kiswahili kibakie kuwa ni alama ya utambulisho, kwa Watanzania na kwa Waafrika. Kiingereza kinapingwa kuwa kisiendelee kuwa lugha ya kufundishia sio ati wananchi wameshindwa kukifahamu vema, la hasha, hoja ni kuwa ni muhimu, na pengine ni lazima Waafrika tuwe na lugha ya utambulisho wetu kama Waafrika. Tumalizie makala hii kwa msemo wa Kiafrika kuwa: Usinga wa kuazima hauwezi kupunga mashetani.

Sehemu ya Nne : Mustakabali na Nafasi ya Kiswahili Kitaifa

Kazi kubwa ya Kiswahili ni kuwaunganisha wasomi na jamii pana ya wananchi, Waafrika. Lugha ya Kiswahili inafanya kazi ya kuwaunganisha wananchi vijijini na watoto wao, wajukuu wao, ndugu zao walioko shuleni, na katika ulimwengu wa kazi. Ulimwengu wa Wasomi unachangamana na ulimwengu wa wenye elimu pana vijijini ili kwa pamoja kuleta Maendeleo. Kutangazwa kwa maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani (UNESCO, Novemba 2021) kuwa iwe tarehe 7 Julai kila mwaka, ni moja ya nguzo muhimu katika hoja yetu ya umuhimu na nafasi ya Kiswahili duniani.

Ni muhimu kwa Serikali kutenga fedha ili kuanza kukitumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia na kujifunzia. Pendekezo la makala hii ni kuanza kwa awamu katika ufundishaji wa masomo katika lugha ya Kiswahili. Tunaweza kuanza kwa masomo ya Insia na kwa vidato vya kwanza na pili. Baada ya muda inaweza kufanywa tathmini ya ujenzi wa maarifa na kujitegemea kwa wanafunzi waliofundishwa kwa kutumia Kiswahili. Baada ya tathmini, inapimwa hali ya kujiamini, kupenda kusoma, kufahamu mambo kwa upana wake n.k. Bilashaka hatua hii itakuwa na mafanikio katika uelewa na kuwa na maarifa, ukweli utakaokiingiza Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika elimu ya sekondari katika vidato vya tatu na nne. Hatua kwa hatua wanafunzi watapimwa na kiwango chao cha kuwa na maarifa kitafahamika. Mfumo huu utaendelea hadi kufika elimu kutolewa vyuoni kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hatua kwa hatua kutoka katika masomo ya Insia, kuingia katika sayansi za jamii na baadaye katika masomo ya sayansi, uhandisi na utabibu.
Lugha ya Kiingereza itabaki kufundishwa kama somo. Walimu walio mahiri katika ufundishaji wa Kiingereza kama lugha ya kigeni, wataachiwa nafasi ili waifundishe vizuri, na wasiingiliwe ili kazi yao iwe na matokeo mazuri inavyotarajiwa. Wanafunzi watajengewa misingi imara na kuhimizwa kusoma lugha nyingine za kigeni kama Kifaransa, Kichina, Kiarabu, Kihispaniola na kadhalika. Mfumo huu utawafanya wanafunzi kufahamu Kiingereza na kuwa na uwezo wa kukitumia katika kuwasiliana na wenzao nchi za nje, au kuandika na kuchapisha tafiti zao au uvumbuzi wao. Watachangia maarifa mapya ambayo yataibuliwa kutokana na kuelewa kwao na kuwa na maarifa na akili ya udadisi na ugunduzi waliyojengewa kwa vile walitumia lugha ya kujifunzia wanayoifahamu na kuimudu.

Hitimisho: Nini kifanyike sasa

Kama alivyosema Maricic, (2007) ikiwa tunataka kukuza uwezo wa wanafunzi wetu wa kuchakata maarifa, ile lugha wanayoitumia kila siku, wanayoitumia kufikiri ni lazima itumike katika elimu. Utumiaji wa Kiswahili utaongeza maarifa na udadisi kwani mwanafunzi atahusisha anayojifunza darasani na mazingira yake mahali anapotokea na vitu anavyoviona kila siku katika maisha yake kwa ujumla. Utumiaji wa Kiswahili utarejesha maadili ambayo yanaporomoka sasa katika jamii; utaongeza uzalendo na kuwajibika kwa mtu kwa taifa lake. Ukweli ni kuwa, Kiswahili kinatumika kufundishia. Tuamue sasa kuwa wanayoyafanya walimu ni sahihi na Mfumo urasimishwe. Serikali itimize lengo lililopo katika Sera ya Elimu ya 2014, kuwa "itatumia lugha ya kiswahili katika ufundishaji" (Sera ya Elimu, 2014: 38). Serikali iwekeze na kukamilisha Tamko la Sera ya Elimu ya 2014, namba 3.2.19 kuwa:

> *Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa (uk. 38).*

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 18 06/07/2023 12:15 PM

Haya yakifanyika, nchi itashuhudia kupanda kwa ubora wa elimu, wananchi wake watakuwa na maarifa na uelewa mpana wa mambo na watakuwa wachangiaji wazuri katika kukua kwa uchumi wa Taifa. Kwa ujumla, MAENDELEO YA UJIFUNZAJI NA UFUNDISHAJI YATAONEKANA WAZI.

MAREJELEO

1. Ashcroft, B., Griffiths, G. na Tiffin, H. Wahr. (2003). The Post-Colonial Studies Reader Routledge, London
2. Azmi, L.N.M. (2013). National Language Policy and Its Impacts on Second Language Reading Culture. Journal of International Education and Leadership. Juz.3. No 1. Kur. 1 – 11. http://www.jielusa.org
3. Bagheri, F. (2015). The Relationship between Critical Thinking and Language Learning Strategies of EFL Learners. Journal of Language Teaching and Research. Juz. 6 No. 5. Kur 969 – 975. DOI: 10.17507/jltr.0605.08
4. Barrett, J. (1994). Why is English still the medium of education in Tanzanian secondary schools? Language, Culture and Curriculum, Vol. 7. No.1, Kur. 3-16, DOI: 10.1080/07908319409525162
5. Brock-Utne, B. (2007). Learning through a familiar language versus learning through a foreign language—A look into some secondary school classrooms in Tanzania. International Journal of Educational Development. Juz. 27. No. 5. Kur. 487-498. DOI: 10.1016/j.ijedudev.2006.10.004
6. Brock-Utne, B. (1993). "Language of Instruction in African Schools — a Socio-cultural Perspective." Nordisk Pedagogik, 4, pp. 225–47.
7. Brock-Utne, B. (2000). Whose Education for All? The Recolonization of the African Mind. New York/London: Falmer Press.
8. Brock-Utne, B. (2001). "Education for All – In Whose Language?" Oxford Review of Education, 27, 1. pp.115–34.
9. Brock-Utne, B. (2002). "The Use of African Languages – a Question of Learning and a Question of Democracy." Revue Gabonaise des Sciences du Langage, 1
10. Criper, C., na Dodd, W. (1984). Report on the Teaching of English language and Its Use as a Medium of Education in Tanzania. Dar es Salaam: British Council
11. Fanon, F. (2008). Black Skin, White Masks. Pluto Press. London
12. Gaddis, I. na Hoogeveen, J. (2015). Primary Education in Mainland Tanzania: What Do the Data Tell Us? 10.1596/978-1-4648-0590-5_ch2. Katika Kitabu: Josh, A.R na Gaddis, I. Wahr. Preparing the Next Generation in Tanzania: Challenges and Opportunities in Education. World Bank Publication (kur.7-25).
13. Hinton, M. (2019). Language and Argument: a Review of the Field. Research in Language. Juz. 17. No. 1. Kur. 93 – 103. DOI: 10.2478/rela-2019-0007
14. Janus, H. na Keijzer, N. (2015). Big Results Now? Emerging Lessons from Results-Based Aid in Tanzania. SSRN Electronic Journal. DOI: 10.2139/ssrn.2673227. German Development Institute. Discussion paper. No 4. Kur
15. Kevogo, S. (2018). Kiswahili katika Kufundishia TEHAMA katika Shule za Msingi nchini Tanzania: Umuhimu na Changamoto zake. Kioo cha Lugha. Juz 13. Kur. 52-64.
16. Kiimbila, J.K. (1971). "Matumizi ya Kiswahili Nchini, Shuleni na Vyuoni". Katika, Kichocheo cha Uchunguzi wa Kiswahili. TUKI, Dar es Salaam.
17. Klaus, D. (2001). "The Use of Indigenous Languages in Early Basic Education in Papua New Guinea: A Model for Elsewhere?" Paper presented on 17 March 2001 at the Annual Conference of the Comparative and International Education Society in Washington DC.
18. Lupogo, I. (2014). Language of Instruction: A Challenge for Secondary Schools and Tertiary Institutions in Implementing VET in Tanzania. Journal of Educational Policy and Entrepreneurial Research (JEPER).Juz.1, N0.3. Kur 26- 30
19. Mekacha, R.D.K. (1997). "Language as a Determinant of the Quality of Education: A Rejoinder." Journal of Linguistics and Language in Education, 3. Department of Foreign Languages and Linguistics. Dar es Salaam, pp. 95–105.
20. Mlama, P., na Matteru, M. (1978). Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Katika Elimu ya Juu. Dar es Salaam: BAKITA.
21. Mtallo, G.R. (2015). Teaching and Learning English in Tanzania: Blessing or Curse? A Practical Review of Phan le Ha's Teaching English as an International Language. Katika Journal of Education and Practice Vol.6, No.17. Kur. 118-123. (Mkondoni) www.iiste.org
22. Mulokozi, M.M. (1989). Nafasi ya Kiswahili katika Kufundishia Elimu ya Juu. Makala yaliyotolewa kwenye Kongamano

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 19 06/07/2023 12:15 PM

la Kiswahili la Kimataifa Kuadhimisha Miaka 20 ya BAKITA, Dar es Salaam, 8 Agosti, 1989.
23. Mwinsheikhe, H.M. (2001). "Science and the Language Barrier: Using Kiswahili as a Medium of Instruction in Tanzania Secondary Schools as a Strategy of Improving Student Participation and Performance in Science." Master's thesis for the M.Phil. in Comparative and International Education. Institute for Educational Research, Oslo.
24. Nikoopour, J. Farsani, A.M. na Nasiri, M. (2011). On the Relationship Between Critical Thinking and Language Learning Strategies Among Iranian EFL Learners. Journal of Technology & Education, Juz. 5, No.3. Kur. 195- 200.
25. NUFFIC, (2014). Education system Tanzania. 1st edition, December 2014
26. Pickering, J.M. na Gambi, C. (2018). Predicting While Comprehending Language: A Theory and Review. Psychological Bulletin Juz. 144. No. 10. Kur. 1 – 76. DOI: 10.1037/bul0000158
27. Qorro, M. (2013). Language of instruction in Tanzania: Why are research findings not heeded? International Review of Education (59): 29-45.
28. Royal Norwegian Embassy, Dar es Salaam: "Politikk og økonomi i Tanzania." Skriv no.58, 22 April 1992, to the Norwegian Foreign Ministry.
29. Roy-Campbell, Z.M. na Qorro, M.A.S. (1997). Language Crisis in Tanzania. The Myth of English versus Education. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
30. Rubagumya, C. (2010). Teaching and Learning English in Africa: Do Learners Matter? Keynote address delivered at the SUZA Spine International Symposium. Zanzibar.
31. Rubagumya, C. (1997). "Disconnecting Education: Language as a Determinant of the Quality of Education in Tanzania." Journal of Linguistics and Language in Education, 3. Department of Foreign Languages and Linguistics, University of Dar es Salaam, pp. 81–93.
32. Senkoro, F.E.M.K. (2007). Mauaji Halaiki ya Watoto wa Tanzania Kupitia Katika Lugha ya Kufundishia Sekondari na Vyuoni. Katika Senkoro, F.E. (mh.) Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki. Dar es Salaam: Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki. Kurasa 39 – 44.
33. Tibategeza, E. na Du Plessis, L. (2018). The Prospects of Kiswahili as a Medium of Instruction in the Tanzanian Education and Training Policy. Journal of Language and Education. 4. 88-98. 10.17323/2411-7390-2018-4-3-88-98.
34. Tibategeza, E na Du Plessis, T.L. (2010). Implementation of Bilingual Education in Tanzania: The Realities in the Schools. Canadian Journal of African Studies. Vol. 19. No. 4. Kur: 227-249
35. Tunçel, H. (2015). The relationship between self-confidence and learning Turkish as a foreign language. Educational Research and Reviews Juz. 10 No.18. Kur. 2575 – 2589. DOI: 10.5897/ERR2015.2445
36. Unesco, 1985: African Community Languages and their Use in Literacy and Education. Dakar: Breda. University of Dar es Salaam (UDSM), 1994: University Screening Test Results for 1994/95. CSU/UDSM: October 1994.
37. Vance, N. (2000). Imperial Rome and Britain's Language of Empire 1600–1837. History of European Ideas. Juz. 26. Na 3-4. Kur. 211-224
38. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2014). Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar es Salaam.

Kutoka kwenye Tovuti mbalimbali

1. http://dar24.com/kwa-nini-shule-za-serikali-zinaongoza-kwa-ufaulu-mbovu-mitihani-ya-taifa/. Imesoma Julai 9, 2022
2. https://www.tamisemi.go.tz/new/msiwaadhibu-walimu-kwa-matokeo-mabaya-a-wanafunzi-nzunda. Imesomwa Julai 9, 2022
3. Mwassa https://www.thecitizen.co.tz/Special-Reports/1841668-2669450-eviwmo/index.html
4. Ndalichako,The Citizen, 2019. https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/english-to-remain-as-a-medium-of-instruction-in-tanzanian-schools-2684080
5. HAKIELIMU, (2017). Strategic Plan 2017-2021. Mkondoni, katika https://d1wqtxts1xzle7.cloudfront.net/53890668/HAKIELIMU_2017-2021_Strategy_Plan-libre.pdf?1500376970=&response-content
6. Carlitz, R. na McGee, R. (2013). Raising the Stakes: The Impact of HakiElimu's Advocacy Work on Education Policy and Budget in Tanzania. IBP Study No. 12, June 2013. Online at https://internationalbudget.org/wp-content/uploads/HakiElimu-Case-Study.pdf
7. Mosenda, J. (2022). Language of instruction in Tanzanian schools continue to draw debate. The Citizen, Saturday June 11 2022. Online at https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/language-of-instruction-in-tanzanian-schools-

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 20 06/07/2023 12:15 PM

continue-to-draw-debate--3845488

8. Mafuruki, A.A (2015). In a globalised world, looking inward is the wrong way to turn. The Citizen, Wednesday March 04 2015. Online at: https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/oped/mafuruki-in-a-globalised-world-looking-inward-is-the-wrong-way-to-turn-2523070
9. Kanyabwoya, D. (2021). TZ@60: Issues that are still pending in Tanzania's education system. The Citizen, Wednesday December 08 2021. Online at: https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/tz-60-issues-that-are-still-pending-in-tanzania-s-education-system-3645614
10. Scudder, C. (2022). Texas Republican leaders' response to the mass shooting: more guns in schools. The Guardian, May 25th. https://www.theguardian.com/us-news/2022/may/25/texas-school-shooting-republican-leaders-respond
11. Weston, M. (2016). How English-medium education is hobbling Tanzania's children. Global Dashboard. https://www.globaldashboard.org/2016/08/22/english-medium-education-hobbling-tanzanias-children/
12. White house (2022). https://www.whitehouse.gov/briefing-room/speeches-remarks/2022/05/24/remarks-by-president-biden-on-the-school-shooting-in-uvalde-texas/
13. Twaweza, (2015). Muhtasari Na. 24. Mkondoni https://twaweza.org/wp-content/uploads/2021/02/Education-FINAL-SW.pdf Imesomwa Julai 10
14. Kenny, E. (2005). "A log in water never becomes a crocodile": practices of return migration and intergenerational gifting in West Africa. Unpublished PhD Thesis. University of Kentucky. DOI:10.13140/RG.2.2.24638.28481. Online at https://www.researchgate.net/publication/34481221_A_log_in_water_never_becomes_a_crocodile_practices_of_return_migration_and_intergenerational_gifting_in_West_Africa
15. Spagat, E. na Coronado, A. (2022) 'Precious individuals' taken in Texas school shooting AP News. Of 3 June. At https://apnews.com/article/victims-uvalde-texas-school-shooting-958714229cac5f6711270301569ccf7a
16. SamplePosts https://www.sampleposts.com/200-african-proverbs-and-their-meaning
17. NPR.ORG (2022). https://www.npr.org/2022/05/25/1101256376/leaders-reaction-to-uvalde-school-shooting-texas-zelenskyy-pope-trudeau
18. Mihyo, P.B, Mmari, D.E, na Msami, J.B. (2021). Uwiano Kati ya Aina ya Kazi, Taarifa Kuhusu Kazi, Stadi za Kazi, na Elimu. Dokezo la Utafiti Na. 1. REPOA. https://www.repoa.or.tz/wp-content/uploads/2021/04/DOKEZO-Toleo-No-1-2021.pdf
19. Cai, M. (2022). Texas has had eight mass shootings in the past 13 years, while lawmakers have steadily loosened restrictions on carrying firearms. The Texas Tribune, May 31, 2022. https://apps.texastribune.org/features/2019/texas-10-years-of-mass-shootings-timeline/

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 21 06/07/2023 12:15 PM

Kiswahili ni Lugha ya Taifa: Kwa nini sio Lugha ya Kufundishia?

Humphrey P. B. Moshi
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

IKISIRI

Kasi ya umaarufu na mvuto wa lugha ya Kiswahili inazidi kuongeza duniani. Hali hii inajidhihirisha wazi kutokana na ongezeko la idadi ya watu wanaoizungumza na kujifunza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Bara la Afrika. Hata hivyo, pamoja na kuwa Tanzania imekuwa kitovu cha asili na wazungumzaji wa Kiswahili, kuna hofu katika kuipa hadhi ya juu kama lugha mama ya kujifunza, kufundishia na kuambukiza maarifa katika ngazi zote za elimu nchini. Aidha, zipo sababu nyingi zilizosababisha hali hiyo ; zikiwemo zile za kasumba, ukimya wa Dira za Taifa za Maendeleo na Sera za Elimu, na suala zima la hofu ya kwamba jambo hilo haliwezekani. Aidha, uchambuzi kwenye mada hii unaweka bayana kwamba hofu hiyo haina mashiko kwa sababu tafiti zinaonyesha wazi kwamba Kiswahili kimeweza, kimsamiati, kwenda na wakati kulingana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia duniani. Hivyo basi, ni vema kuachana na hizo dhana potovu na kuanza maandalizi chanya ya kuipa lugha ya Kiswahili hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia. Wakati huo huo, maamuzi ya mchakato wa maandalizi hayo ni lazima yaainishwe wazi wazi kwenye Dira ya Maendeleo 2025-2050 na kwenye Sera husika za Elimu.

UTANGULIZI

Ni ukweli usiofichika kwamba lugha ya Kiswahili imekuwa sana nje na ndani ya Bara la Afrika. Halikadhalika kimataifa jumuiya mbalimbali za Kiafrika na zikiwemo zile za Afrika Mashariki (EAC) na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Vilevile, shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) katika Kikao chake cha 41, Novemba 2021 wameitambua lugha hiyo na kufanya uamuzi wa kuiadhimisha tarehe saba (7) Julai kila mwaka, chini ya kaulimbiu "Siku ya Kiswahili Duniani"

Wakati huo huo, vyombo vya habari katika nchi nyingi duniani, zikiwemo Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, China n.k. vinatangaza vipindi maalum vya radio na televisheni (Runinga) kwa lugha ya Kiswahili. Vyombo hivyo ni pamoja na : Deutsche Welle, BBC, CRI Kiswahili, n.k. Aidha, zaidi ya watu milioni 150 wanazungumza lugha hiyo kwa sasa duniani. Lakini cha kushangaza Tanzania, ambayo sio tu ni chimbuko na kitovu cha Kiswahili, bali pia waliifanya Kiswahili kuwa lugha ya Taifa, haijaipa hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia katika nyanja zote za elimu. Kutokana na hali hii, lengo kuu la mada hii ni kujaribu kutafuta sababu zilizosababisha kuwepo kwa kitendawili hicho.

Aidha, katika kutimiza lengo hili, mada hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Baada ya utangulizi huu, kipengele kinachofuata kitachambua sababu ya kitendawili hicho. Sehemu ya tatu itajikita kwa kujibu swali, Je jambo la kukifanya Kiswahili lugha ya

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 22 06/07/2023 12:15 PM

kufundishia linawezekana ? Kama jibu ni ndiyo, sehemu ya nne itapendekeza ni nini kifanyike ili kufikia azma hiyo. Sehemu ya mwisho itahitimisha mada kwa kisisitiza umuhimu wa kufanya maandalizi chanya.

Tatizo lipo Wapi?

Mwezi wa Juni, 1979 wakati wa ufunguzi wa Taasisi ya Kiswahili ya Zanzibar, Mwanduh Ahmed Mgeni aliandika katika jarida la "New African", ukurasa wa 76, na kukiri kwamba "Kiswahili kinaendelea kupata hadhi ya kimataifa duniani". Pia alidokeza kwamba UNESCO ilikuwa tayari kutumia Kiswahili kama mojawapo ya lugha zake rasmi. Hatimaye, alishukuru Baraza la Kiswahili la Taifa, na Taasisi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kukuza na kusambaza lugha hiyo katika nyanja mbalimbali. Pamoja na juhudi hizo, chakushangaza ni kwamba, kwa nini hadi leo hii lugha hajapewa hadhi ya kuwa ya kufundishia vyuoni? Zipo sababu kadha ambazo tutazichambua katika vipengele vinavyofuata

Ulimbukeni/kasumba: Bado kuna hali ya kupenda vya nje kuliko vya ndani. Sio kwenye swala la lugha tu, bali hata katika matumizi ya bidhaa. Aidha usomi au kuonekana umesoma kuna fikra kuwa ni lazima ujue au uzungumze kimombo kidogo yaani Kiingereza. Hali hiyo ililetwa na ukoloni na baadae ukoloni mamboleo ambao ulilenga kufuta au kudharau mila na desturi za asili walizozikuta kwenye nchi zetu na bara letu la Afrika. Aidha, mila na desturi hizo zilionekana machoni pao kwamba ni za "kishenzi" au sio za kistaarabu. Lakini, cha kushangaza ni kwamba, hata baada ya nchi hizo kupata uhuru wa kisiasa, bado fikra hizo potofu zimeendelea kuwepo na kusababisha watu kudharau vitu vya nyumbani na kupapatikia vile vya kutoka nje; hata kama vitu vya nyumbani ni bora kuliko vya nje.
Kasumba hii inaonekana dhahiri kwenye suala zima la lugha za asili, ikiwa ni pamoja na lugha ya Kiswahili. Hivyo kusababisha wapenzi wa lugha hizo, wakiwepo wataalamu, kujiuliza "kulikoni". Kwa maana kwamba: Kwa nini tunakuwa na ukakasi au hofu kwenye hili?

Ukimya wa Dira za Taifa za Maendeleo: Mbali na suala la kasumba, ukimya katika Dira za Maendeleo, umechangia sana katika hali ya kutokuthamini na kuipatia hadhi yake lugha ya Kiswahili. (Azimio la Arusha, 1967; Dira 2025, 1999). Itakumbukwa kwamba, Dira hizo za Maendeleo ya Taifa zilikuwa kimya kwenye kutamka waziwazi kwamba Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia. Kimsingi maendeleo ya kuichumi na kijamii nchini mwetu, kuanzia miaka ya sitini, mara baada ya kupata Uhuru, yaliongozwa na misingi ya Dira iliyobainishwa katika Azimio la Arusha (1967). Hususan, Dira hiyo ililenga kujenga jamii yenye kuthamini UTU wa Mwanadamu, USAWA katika mahitaji ya msingi na hivyo kuwa na UHURU wa kujiamulia mambo yake bila kuingiliwa.

Katika kutekeleza Dira hiyo, ni mambo mengi yaliyofanyika, zikiwemo juhudi nyingi za kuendeleza lugha ya Kiswahili, kama kuijenga kuwa lugha ya Taifa. Lakini bado juhudi hizo hazikutamka wazi kuhusu lugha ya Kiswahili kuwa ya kufundishia kwenye vyuo vya elimu ya juu.

Kuanzia mwaka 1986, Tanzania ilifanya mageuzi makubwa katika sera na mikakati ya kuleta maendeleo ya jamii (Benki ya Dunia, 1981). Pamoja na mageuzi hayo, ilibainika kuwa mageuzi hayo yalikuwa yakifanyika bila kuwa na dira na misingi iliyokubalika na jamii nzima. Hivyo basi, na kwa nia ya kuziba pengo lililoachwa na Dira ya Azimio la Arusha, mchakato wa kutayarisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ulianza mwaka wa 1996. Pamoja na mchakato huo kushirikisha vikundi mbalimbali vya jamii, vikiwemo vile vinavyoshughulika na mambo ya utamaduni na maendeleo, swala la umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia halikujitokeza waziwazi. Kwa mantiki hiyo, bado swali la: kwa nini hali imekuwa hivyo? Halijapata jibu.

Sera za Elimu: Katika Tanzania zimekuwapo sera mbalimbali zinazogusa au kuzungumzia utamaduni au elimu. Kwa mfano, kumekuwapo Sera ya Elimu na Mafunzo (1995); Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo (1996); Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu (1999); sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa elimu msingi (2007); na Sera ya Elimu na Mafunzo (2014). Sera zote hizo zililenga kuboresha mazingira ya utoaji elimu na mafunzo kwa lengo la kupata Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mtazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Pia sera hizo zilisisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza, alama na lugha nyingine za kigeni. Hata hivyo, hakuna mkakati madhubuti ulioandaliwa kuwezesha Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundisha baada ya elimu ya msingi

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 23 06/07/2023 12:15 PM

Je Jambo hili linawezekana ?

Bila hofu, wala kigugumizi jibu ni "ndiyo" kwa sababu kuu mbili zifuatazo:

Lugha imeweza kwenda na wakati: Moja ya hofu au wasiwasi zilizokuwa zinatolewa na wadau wengi, kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili ni kwamba haina misamiati ya kutosha kukidhi mahitaji ya dunia inayobadilika badilika. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba hofu hiyo haina mashiko.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko mengi duniani kwenye nyanja mbalimbali, hususani uchumi na teknolojia. Aidha, katika hali hiyo, lugha ya Kiswahili ilimudu kwenda na wakati kwa kuwa na misamiati ambayo inaainisha barabara fursa na changamoto zinazojitoza kwenye mazingira hayo mapya. Baadhi ya misamiati hiyo ni pamoja na: utandawazi, kingamuzi, kisimbuzi, barua pepe, tovuti, Vocha, simu janja, kidigitali, tabia nchi, UVIKO-19 na mengineyo mengi.

Aidha, ni lazima tukubali ukweli kwamba lugha, zote duniani, zinaingiliana na kubebana, na mara nyingi huazimana (kukopeshana maneno). Hali hiyo imetokana na upana na urefu wa utandawazi. Kwa mantiki hiyo, cha msingi sio ladha tu ya msamiati husika au uasilia wake, bali ni uelewa sahihi wa kupata na kufikisha ujumbe husika au uliokusudiwa kwa mlengwa.

Kwa mfano, neno "mtori" ni aina fulani ya chakula cha kabila la kichaga. Lakini kwa sasa, hakuna kabila lolote Tanzania ambalo halitumii jina hilo, au kukitumia chakula hicho. Hii ni kuonesha kuwa lugha inapata msamiati kutoka katika lugha mbalimbali za kiafrika. Halikadhalika, chakula aina "Chips" linatumiwa na makabila mengi nchini Tanzania na hata nje ya Tanzania. Kamusi ya Oxford English katika Toleo lake la Juni, 2022, imeweka maneno kadhaa ambayo kimsingi ni kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno kama chips mayai, sasa ni msamiati katika lugha ya Kiingereza. Hivyo, neno « chips » linalotumika katika Kiswahili asili yake ni Kiingereza. Mifano hii, ni kielelezo tosha ya kwamba hakuna lugha inayojitosheleza yenyewe.

Machapisho mbalimbali ya Kiswahili : Kumekuwepo na machapisho mengi mbalimbali ya Kiswahili. Machapisho hayo yametafsiriwa kutoka Kiingereza au yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili moja kwa moja. Kwa mfano, hotuba za bajeti za kila wizara, zinazowasilishwa Bungeni na Waziri husika, huchapishwa na kuwasilishwa kwa Kiswahili na kiingereza. Hivyo hivyo, taarifa za mwaka, za taasisi na sekta mbalimbali huchapishwa kwa lugha hizo mbili. Huo ni uthibitisho tosha kwamba yote yanawezekana mradi tu kuna nia thabiti. Hapa tunaweza kurejelea msemo wa Kiswahili : penye nia pana njia. Hivyo basi, hofu na kusitasita kwenye jambo hili hazina sababu za msingi.

Nini kifanyike ?

Tanzania katika miaka ya usoni itakuwa nchi ya viwanda na utalii. Hivyo ni fursa kubwa kukiwezesha Kiswahili sasa ili kiwe lugha yenye kuwa na mawanda mapana kwakuwa nchi yetu itazidi kujulikana duniani, kadri ya kina cha utandawazi kinavyozidi kuongezeka na uchumi kuimarika. Ikumbukwa kwamba kuna uhusiano wa karibu sana kati ya kukua kwa uchumi na umaarufu wa nchi husika. Kwa mfano, kukua kwa Uchumi wa China kumepelekea nchi hiyo kuwa na taasisi ya Confucius inayoratibu mafunzo ya lugha ya Kichina. Kwa sasa kuna taasisi kama hizi 162 katika nchi mbalimbali duniani. Lugha ya Kichina inaipa nguvu ya kiutamaduni ambapo kupitia kwayo, inaongeza nguvu ya kiuchumi. Hivyo basi, huu ni wakati muafaka wa kuendeleza lugha letu, hususani kuifanya kuwa lugha ya elimu na mafunzo, ili hatimaye iweze kuujenga na kuukuza uchumi wetu. Katika mawazo haya, ni vema kufanya yafuatayo:

Mosi, kuachana kabisa na fikra za ulimbukeni (kasumba) ya kwamba kuelimika au kuwa msomi ni lazima kutumia lugha ya kigeni kufundishia. Lililo muhimu ni kuwapa wanafunzi maarifa kupitia katika lugha wanaoijua vizuri ; na kuwaacha wajifunze lugha nyingi za kigeni kama masomo darasani.

Pili, maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025/2026 -2049/2050 iliweke bayana suala hili kwenye maazimio yake. Aidha, hatua zilizochukuliwa na Waziri wa Fedha, katika bajeti yake ya hivi karibuni (Juni 2022), ya kwamba Kiswahili sasa kitumike kwenye usaili wa kazi.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 24 06/07/2023 12:15 PM

Aidha, siku chache zilizopita, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, aliagiza kwamba 'kuanzia sasa nyaraka zote za Serikali zikiwemo mikataba na miradi mbalimbali zitakuwa zikiandikwa kwa Kiswahili. Pia lugha hiyo inapaswa kutumika katika dhifa zote za Taifa, semina, warsha na mijadala ya umma' (Mwananchi, 08.07.2022, Uk. 2). Hatua zote hizi ni habari njema katika kuendelea kukienzi na kukikuza Kiswahili, lakini lengo kuu liwe lile la kukifanya lugha ya kufundishia. Hivyo basi, ni vema viongozi watamke lengo hilo wazi wazi.

Tatu, pale inapowezekana, hotuba za viongozi wetu, wakati wakiwa kwenye ziara zao nje ya nchi, ziwasilishwe kwa Kiswahili, ili kukifanya Kiswahili kusikika na kujulikana zaidi kwa upande mmoja, lakini pili kuwapa watu ajira kupitia ukalimani na tafsiri za hotuba na nyaraka za Kiserikali nchi za nje

Nne, katika siku za karibuni, kuna wanaharakati wengi wa Afrika ya Kusini wanaohamasisha wadau wengine wapigie dede lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Bara la Afrika. Kwa mantiki ya kuwa na lugha moja Barani mwetu kwa nia ya kupambana au kuondoa mgawanyiko ulioletwa na ukoloni. Hiyo basi, ni vema viongozi wa Tanzania wawe mstari wa mbele wa kuunga mkono juhudi hizo za ukombozi, kama ilivyokuwa katika ukombozi wa kuondoa kutawaliwa kusini mwa Afrika ; na kupiga vita ubaguzi wa rangi Afrika ya Kusini.

Tano, aidha, katika maadhimisho ya mwaka huu ya "Siku ya Kiswahili Duniani 2022", Serikali kwa kupitia Waziri wa Utamaduni na Michezo Bw. Mohamed Mchengerwa, ilitangaza kwamba imetenga eneo lenye ekari mia moja katika Wilaya ya Bagamoyo, kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kiswahili, kwa madhumuni ya kueneza lugha ya Kiswahili duniani. Ukweli ni kwamba, hatua hiyo ni mwanzo mzuri lakini haitoshi ; ni vema Chuo hicho pia kikabebeshwa jukumu la kuhamasisha umuhimu wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu nchini.

Sita, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) wawezeshwe zaidi, kifedha n.k., ili waboreshe uwezo wao wa kuzalisha maneno na misamiati mipya kwa nia ya kukidhi mahitaji ya kufundishia masomo mbalimbali nchini.

Saba, pamoja na hayo, lugha za kigeni (Kiingereza, Kichina, Kifaransa, n.k.) ziendelee kufundishwa kama somo kwa matakwa ya watu binafsi, vikundi au sababu nyingine muhimu, ili kukidhi mahitaji ya utandawazi ambayo yanasababisha nchi kutegemeana kiuchumi, kibiashara, kiteknolojia, kisiasa na kiutamaduni.

Hitimisho

Makala hii imeelezea nafasi ya Kiswahili katika hali ya dunia ya sasa. Nafasi ambayo inadhihirisha wazi kwamba, hadhi ya Kiswahili inakuwa kwa kasi duniani. Makala imehoji kuwa cha kushangaza ni kwamba ijapokuwa lugha hiyo kitovu chake ni Tanzania, bado nchi hii haijaifanya lugha hii kuwa ya kufundishia kwa sababu mbalimbali, zikiwemo kasumba na kutopewa kipambele kwenye Dira za Taifa za Maendeleo na Sera ya Elimu na Mafunzo.

Aidha, tumeonesha kuwa Kiswahili kimedhihirisha kwamba kinakwenda na wakati, kwa kuenea, kwa kuongezeka msamiati, kwa kufafanua masuala ya kiteknolojia na kuwa kwa sasa kina mvuto mkubwa duniani. Ni wazi kwamba wakati ni huu wa kufanya yale ambayo tulishindwa kuyatekeleza siku za nyuma. Lakini utekelezaji wa azma hii, usidhoofishe juhudi za kujifunza lugha nyingine za kigeni na hata kuzitumia katika mawasiliano na ulimwengu wa nje, kwani zinahitajika sana kuifanya Tanzania iendelee kuwa na mawasiliano na ushirikiano wa kidiplomasia na kibiashara hasa wakati wa zama hizi za utandawazi.

MAREJELEO

Benki ya Dunia (1981) : Kuongeza Kasi ya Maendeleo Barani Africa, Washington, D.C.
Gazeti la Mwananchi (2022) : 'Mpango : Nyaraka za Serikali, Mikutano kwa Kiswahili', Tarehe 08.07.2022, Uk. 2, Dar es Salaamhttps://thisisafrica.me/africans-rising/malema-calls-for-swahili-as-africa-common-language/ https://www.youtube.com/watch?v=i-GHJGtLzvE)

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 25 06/07/2023 12:15 PM

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (199): Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Dar es Salaam
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1967). Azimio la Arusha, Dar es Salaam
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995). Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar es Salaam, Tanzania:
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1999). Sera ya Elimu ya Juu. Dar es Salaam
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2022). Bajeti ya Mwaka 2022/2023, Dar es Salaam
Wizaya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WyEMU). (2014). Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar es Salaam, Tanzania:

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 26 06/07/2023 12:15 PM

Kuboresha Ufundishaji wa Kiingereza Katika Shule za Sekondari Tanzania: Umuhimu wa Kuzingatia Maelekezo ya Nadharia

Martha Qorro
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Utangulizi

Kabla ya kuzungumzia mbinu za kuboresha ufundishaji wa Kiingereza kama lugha, ni vema kutazama matatizo yanayoikabili ufundishaji wa lugha hiyo katika shule za sekondari nchini Tanzania hivi sasa. Matatizo hayo ni pamoja na: kutowekwa maanani maelekezo ya nadharia za kufundisha/kujifunza lugha ya pili au ya kigeni; na sera ya lugha katika elimu kutozingatia suala zima la kufanikisha mawasiliano katika jamii ya Watanzania wakati wa kupanga na kuamua lugha ipi itumike kufundishia. Matatizo haya mawili yanaonekana kuzaa mazingira ya kukwamisha badala ya kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza. Mazingira hayo ni pamoja na malengo yasiyo wazi ya kufundisha Kiingereza iwapo ni lugha ya pili au ya kigeni; matumizi ya Kiingereza kibovu kufundishia masomo mengine; kukatazwa matumizi ya lugha za awali; kuwepo kwa vitabu vya ngazi isiyo mwafaka kwa wanafunzi; na walimu wasiofuzu vema katika kufundisha Kiingereza. Pamoja na mambo haya, makala hii pia itapitia nadharia kadhaa zinazoongoza ufundishaji wa lugha ya pili au ya kigeni; na italinganisha ufundishaji wa Kiingereza Tanzania na katika nchi zingine zinazofundisha Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni. Makala hii itaanza kwa kuzungumzia hali ilivyo sasa na athari zake; na pia namna ya kukabili athari hizo kwa kuzingatia kauli ya Sera ya Elimu kuhusu nafasi na matumizi ya Kiingereza katika elimu na katika jamii ya Tanzania. Makala itahitimisha kwa kueleza njia mbali mbali zinazoweza kutumiwa ili kuboresha ufundishaji wa Kiingereza na kutoa mapendekezo kuhusu nini kifanyike ili kuboresha ufundishaji wa Kiingereza.

Ni muhimu tunapozungumzia kuboresha ufundishaji wa Kiingereza (lugha lengwa) kuzingatia na kuweka maanani mazingira ambayo Kiingereza kinapofundishwa na uwepo wa lugha za awali kama vile lugha za asili na Kiswahili. Nchini Tanzania kuna lugha zaidi ya 150 za makabila mbali mbali ambazo ndizo lughamama, au lugha ya kwanza kwa walio wengi; pia kuna Kiswahili

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 27 06/07/2023 12:15 PM

ambayo ni lugha rasmi na lugha ya pili kwa Watanzania wengi. Zaidi ya hapo kuna lugha ya Kiingereza ambayo pia ni lugha rasmi. Katika makala hii kuna dhana zinazotajwa mara kwa mara kama vile lughamama au lugha ya kwanza, lugha ya pili na lugha ya kigeni. Kabla ya kuendelea ni vema kuzifafanua dhana hizi kama zilivyotumika katika makala hii, ikifuatiwa na maelezo mafupi kuhusu ufundishaji wa Kiingereza inapokuwa lugha ya kwanza, lugha ya pili au lugha ya kigeni. Ufafanuzi huo utatuwezesha kuelewa ufundishaji wa Kiingereza nchini Tanzania unafaa kuakisi mazingira yapi: ya lugha ya kwanza, ya pili au ya kigeni.

Lugha ya kwanza ni ile inayotumika katika mawasiliano ndani ya familia ambako wazazi, walezi na watoto hujifunza na kutumia lugha hiyo tangu utotoni na kuendelea kuwa nayo katika makuzi yake; na wakati mwingine inaitwa Lughamama. Kwa Watanzania wengi, hasa wanaoishi vijijini, lugha ya kwanza ni lugha za asili au lughamama za makabila mbali mbali ambazo hata sasa bado zinatumika kwa mawasiliano, siyo katika ngazi ya familia tu, bali hata katika jamii inayozunguka ndani na hata nje ya kijiji.

Lugha ya pili ni ile ambayo mara nyingi haitumiki katika ngazi ya familia, ila mtoto hukutana nayo anapotoka nje ya familia kama vile anapokwenda shule au katika nyumba za ibada. Wakati mwingine lugha ya pili ni lugha yo yote ambayo mtu anajifunza baada ya lugha ya kwanza. Kwa hiyo mtu anaweza kuwa na lugha ya pili zaidi ya moja, kutegemeana na jinsi anavyoitumia. Kwa Watanzania wengi lugha ya pili ni Kiswahili; lugha ambayo Watanzania wa makabila mbali mbali wanapokutana huitumia kuwasiliana. Wapo watoto wa Kitanzania ambao wanaikuta Kiswahili kwa mara ya kwanza wanapoanza shule. Sifa kuu ya lugha pili ni kutumika katika jamii pana na mawasiliano rasmi; kwa mfano, katika ofisi za serikali, nyumba za ibada, mikutano ya hadhara, usafiri wa barabara; na biashara sokoni, minadani, gulioni, n.k. Nchini Tanzania Kiswahili imechukua zaidi ya miaka 60 na juhudi kubwa za kisiasa kufikia hatua hiyo ya kuwa lugha ya pili kwa Watanzania walio wengi; pia wapo Watanzania ambao Kiswahili ni lugha ya kwanza, hasa wale waishio mijini.

Lugha ya kigeni ni ile ambayo inatumika katika mazingira maalumu anapotokea mgeni ambaye hafahamu lugha ya jamii husika; kwa hiyo inabidi itumike ili kumshirikisha mgeni au kumtafsiria kwa lugha yake. Ni lugha ambayo haitumiki mara nyingi na kwa hiyo haieleweki kwa wengi katika jamii pana. Kwa asilimia kubwa ya Watanzania, Kiingereza ni lugha ya kigeni. Baadhi ya Watanzania, hasa wanaoishi mijini ambao kwao Kiswahili ni lugha ya kwanza, wanaichukulia Kiingereza kuwa ni lugha yao ya pili. Kimahesabu kweli ni lugha yao ya pili; lakini kimatumizi bado hakijafikia kiwango hicho cha kuwa lugha ya pili. Msingi wa tofauti hizi ni matumizi ya lugha zaidi kuliko idadi ya kuwa ni lugha ya ngapi baada ya lughamama. Kwa mantiki hiyo, hali halisi ya matumizi ya Kiingereza nchini Tanzania inafanya ibaki kuwa lugha ya kigeni kwa Watanzania walio wengi.

Lugha za asili, Kiswahili na Kiingereza zote zinatumika katika ngazi mbali mbali za jamii nchini Tanzania (familia, jamii, taifa na kimataifa); pamoja na kuenzi ubayoanuwai wa lugha, kuwepo kwa lugha hizi za asili na Kiswahili ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kama Kiingereza. Akizungumzia umuhimu wa lugha katika ngazi zote za jamii, aliyekuwa Balozi wa Ujerumani nchini Latvia, Bw. Eckart Herold, (2005) alisisitiza mambo matatu muhimu katika kujifunza na kufundisha lugha kuwa ni: kwanza na la muhimu zaidi ni wajibu wa kila mtu kujifunza lugha yake ya asili; la pili, kila mtu ni lazima ajifunze lugha rasmi ya nchi anamoishi ili kufanikisha umoja, mshikamano na uelewa wa pamoja; na la tatu, lugha za kigeni huwa ni changamoto, na ili kila mtu aweze kuwa sehemu ya dunia ni vema kuzijifunza.

Maelezo haya ya Herold (ingawa alizungumzia mazingira ya Ulaya), yanafaa yatiliwe maanani katika nchi za Afrika kwa kuwa, pamoja na lugha za asili kuwa nyingi, uwingi huo usitutishe tukaziacha zikapotea. ubayoanuwai wa lugha ni muhimu kwa kuwa kuna ujuzi mwingi na maarifa tele yaliyobebwa katika hizi lugha za asili; ndiyo maana wenzetu wa Ulaya na Asia hawaruhusu lugha yao yoyote ikapotea. Maarifa na ujuzi tuliojifunza kwa lugha zetu tangu utotoni yanatupanulia wigo wa kujifunza lugha zingine; na hiyo ni vema lugha hizo zikaendelea kuwapo.

Tunapozungumzia kuboresha ufundishaji wa Kiingereza tuzingatie mazingira na hali halisi ya ufundishaji wa Kiingereza katika shule za sekondari nchini Tanzania ambapo lugha nyingine zinatumika. Kwa mfano, wanafunzi wengi wa shule za sekondari za kutwa nchini Tanzania, hasa maeneo ya vijijini wanaishi kwenye mazingira ambayo lugha za asili (Lughamama), Kiswahili na Kiingereza vyote vinatumika kwa nyakati tofauti katika maisha ya kila siku. Ni kweli kuwa Kiingereza kinatumika kufundishia elimu ya sekondari na elimu ya juu nchini Tanzania; lakini ni dhahiri kuwa katika nafasi hiyo Kiingereza kimebebwa na sera ya lugha katika elimu. Katika mazingira ya kawaida, bila sera ya lugha katika elimu kusisitiza matumizi ya Kiingereza pekee, mawasiliano karibu yote yangefanyika bila kutumia Kiingereza. Katika mazingira hayo, tukifanya maamuzi ya kuendelea

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 28 06/07/2023 12:15 PM

kufundisha au kuboresha ufundishaji wa Kiingereza kama lugha ya pili ni dhahiri kuwa hatutafanikiwa au tutakuwa na mafanikio hafifu sana. Jambo hili litafafanuliwa zaidi baadaye katika makala hii. Kwa sasa ni vema kuelezea kidogo tofauti kati ya kufundisha Kiingereza kama lugha ya kwanza, lugha ya pili au lugha ya kigeni.

Ufundishaji wa Kiingereza kama lugha ya kwanza, ya pili au ya kigeni

Mosi, mwanafunzi anayefundishwa Kiingereza kama lugha ya kwanza au lughamama anaifahamu lugha hiyo bara bara, bali anajifunza ili aelewe sarufi, miundo ya maneno na ya sentensi pia historia ya lugha hiyo. Mwanafunzi anatafuta umahiri zaidi wa Kiingereza, mara nyingi ni kwa minajili ya kuifundisha kwa watu wengine wasiyoifahamu Kiingereza. Lugha hii inafundishwa kama lugha ya kwanza katika nchi kama Uingereza, Australia, New Zealand, sehemu za Canada na Marekani (USA).

Pili, mwanafunzi anayefundishwa Kiingereza kama lugha ya pili anakuwa ameshajifunza sehemu kubwa ya lugha hiyo kabla hajaanza shule kwa kuisikia katika jamii anayoishi ambamo ni lugha kuu ya mawasiliano, ingawa kinaweza kuwa na makosa au matumizi yasiyo rasmi au mabovu. Pia anaweza kuwa ameisikia Kiingereza katika vyombo vya habari, redio, luninga, mikutano ya hadhara, ofisi za Serikali na Bunge, biashara za sokoni, madukani na ofisi muhimu kama posta, benki, nyumba za ibada, usafiri na kadhalika. Mifano ya nchi ambazo Kiingereza kinafundishwa kama lugha ya pili ni pamoja na: Ghana, Zambia, Kenya, Uganda, Malawi, Hong Kong, Singapore, Fiji, na zinginezo.

Tatu, mwanafunzi anayefundishwa Kiingereza kama lugha ya kigeni huwa hapati nafasi ya kukisikia na kujifunza isipokuwa katika mazingira ya shule. Anafundishwa Kiingereza kama somo shuleni na anaishi katika mazingira ambamo Kiingereza siyo lugha ya kawaida ya mawasiliano katika familia na katika jamii anamoishi. Mwanafunzi huyu huwa hana fursa ya kujifunza Kiingereza kutoka kwa wazazi wake wala kwa jamii inayomzunguka, bali hufundishwa na hujifunza darasani kwa mwalimu wa somo hilo. Nchini Tanzania mara nyingi mwanafunzi huyu anatoka katika jamii ambamo hakuna uwezo wa kifedha kusoma masomo ya Kiingereza ya ziada (tuisheni), kupata michezo ya video, wala vitabu vya ziada vya Kiingereza; pia kwa kuwa vyote hivi havipatikani kwa wepesi, hasa katika mazingira ya vijijini. Kwa hiyo mazingira ya kufundisha Kiingereza kwa mwanafunzi wa aina hii ni lazima yawe yanajitosheleza kufundisha lugha hiyo kwa usahihi tangu mwanzo. Kinyume chake, matumizi ya Kiingereza kisicho sahihi yatamkwaza mwanafunzi huyu kujifunza Kiingereza. Mazingira ya darasa la kujifunzia Kiingereza kwa mwanafunzi ambaye Kiingereza ni lugha ngeni yanahitaji vifaa vya kufundishia ambavyo ni mwafaka kwa ngazi yake; na mafunzo yanayokwenda hatua kwa hatua kwa kuzingatia kwamba hiyo ni fursa pekee ya kujifunza na kumfundisha Kiingereza vizuri. Mifano ya nchi zinazofundisha Kiingereza kama lugha ya kigeni ni kama vile: Norway, Ufaransa, Italia, Ujerumani, Brazil, Kongo na Senegal na nyinginezo. Tofauti hizi kati ya kufundisha Kiingereza kama lugha ya kwanza, ya pili au ya kigeni zisipotiliwa maanani katika kutunga sera na mitaala, ufundishaji wa Kiingereza hudorora.

Kwanini ufundishaji wa Kiingereza katika shule za sekondari Tanzania umedorora

Hali halisi ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza nchini Tanzania: Pamoja na matatizo yote yaliyotajwa katika utangulizi wa makala hii, ufundishaji wa Kiingereza umedhoofika katika shule za sekondari nchini Tanzania kwa sababu kadhaa. Sababu ya kwanza ni malengo ya kufundisha Kiingereza hayako wazi. Tunafundisha au kujifunza Kiingereza ili tukitumie wapi, au katika maeneo yapi ya maisha ya Watanzania? Mihtasari ya somo hili kwa miongo kadhaa sasa, haiko wazi katika eneo hili. Malengo ya kufundisha Kiingereza yasipokuwa wazi, utekelezaji wake ni dhahiri utakuwa mgumu au utakwama.

Sababu ya pili ni kuwa kutumia Kiingereza kufundishia kunadhoofisha ufundishaji wa lugha hiyo. Hoja hii ni ngumu kukubalika kama vile ukimwelekeza mtu kwamba njia ya kwenda mashariki ni kwenda magharibi kwanza. Wengi wanaamini kuwa kutumia Kiingereza kufundishia kunawapa wanafunzi nafasi ya kukisikia, kukitumia na hatimaye kukijifunza. Wanatumia msemo wa Kiingereza usemao: Practice makes perfect. Lakini ukichunguza zaidi, hali halisi inakinzana na imani au kauli hiyo. Hali halisi ni kuwa, wale walimu wanaotumia Kiingereza kufundisha taaluma zao kama vile: Historia, Jiografia, Hisabati, Biolojia, Kemia, Fizikia, Biashara, n.k. siyo wataalamu wa Kiingereza. Kwa hiyo, mara nyingi hutumia Kiingereza kisicho rasmi au kisicho sahihi, sanifu au fasaha.

Ukiacha somo la Kiswahili, masomo hayo yote na mengine yanafundishwa kwa Kiingereza kisicho sanifu (mifano hai ipo). Hali

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 29 06/07/2023 12:15 PM

hii inawajengea wanafunzi mazingira ya kusikia/kutumia Kiingereza kisichofasaha kwa muda mwingi zaidi kuliko wanavyosikia na kutumia Kiingereza fasaha cha mwalimu wa Kiingereza. Hali hiyo inaathiri au kufuta kabisa Kiingereza fasaha alichofundisha mwalimu wa Kiingereza (mwalimu moja wa Kiingereza kwa kila darasa, ilhali kuna walimu saba au zaidi wa masomo mengine kwa siku kwa darasa hilo hilo). Kwa hiyo, siyo kweli kwamba: practice makes perfect. Badala yake, wanafunzi wakisikiliza na kutumia Kiingereza kibovu kwa walimu wote hawo, hawatajifunza kilicho sahihi, bali watajifunza hicho hicho kibovu. Hata kwa mahesabu ya kawaida: dakika 40 au 80 za kufundishwa Kiingereza sahihi kwa siku (cha mwalimu wa Kiingereza) haziwezi kuhimili au kushindana na dakika 360 au saa sita kwa siku za Kiingereza kibovu (cha walimu wa masomo mengine). Kwa vyo vyote vile, hata kukiwa na mwalimu Mwingereza akafundisha Kiingereza, katika mazingira hayo atakuwa na wakati mgumu kuboresha ufundishaji wa Kiingereza. Kwa hiyo usemi wa: Practice makes perfect unabadilika kuwa: practice makes permanent, kwa kuwa wanafunzi wanakomaa katika kusikia Kiingereza chenye makosa kutoka kwa walimu wao; makosa ambayo kwa miaka sita ya elimu ya sekondari yanakuwa ya kudumu na wanakwenda nayo mpaka vyuoni. Hali hii pia inasababisha maandalizi ya walimu wa somo la Kiingereza kuwa magumu zaidi kuliko ambavyo wangefundishwa Kiingereza kama lugha tu. Pia hali hii inamaanisha kuwa mamlaka ya walimu wa somo la Kiingereza yamekasimiwa kwa walimu wa masomo mengine; hivyo Kiingereza kinakosa wadau wa kukisimamia kwa dhati (cha wote hakina mwenyewe). Katika mazingira haya, hatutakuwa mbali na ukweli tukisema kuwa kutumia Kiingereza kufundishia kunadhoofisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza.

Tatizo lingine linalodhoofisha ufundishaji wa Kiingereza ni utaratibu au mtindo wa kufundisha Kiingereza katika mazingira ambayo lugha zingine haziruhusiwi. Katika shule za sekondari nchini Tanzania kuna sheria inayosema: Speak English Only! No English, No Service! Hali hii inatengeneza ombwe katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiingereza (au lugha nyingine yo yote). Kujifunza ni mchakato wa kujenga uhusiano kati ya vitu au mambo ambayo mwanafunzi anafahamu na mapya asiyoyafahamu. Baadhi au mengi ya mambo anayofahamu yako katika lughamama au Kiswahili. Kama anavyoeleza Mweteni (1996), mwanafunzi anayejifunza Kiingereza, tayari amejifunza lughamama na au Kiswahili, yaani tayari anajua jinsi mfumo wa kanuni na taratibu (code) unavyofanya kazi katika lughamama; na huo mfumo wa kanuni na taratibu anaoufahamu ndiyo unamwezesha mwanafunzi kuuelewa mfumo mpya. Mwanafunzi akifanikiwa kujenga uhusiano huo, ndiyo amejifunza au ameelewa; na asipofanikiwa maana yake hajajifunza au hajaelewa. Kujifunza Kiingereza kunatumia kanuni hiyo hiyo. Kwa maneno mengine, tunapojifunza lugha mpya, penda, tusipende, tunajikuta tunahitaji kutafuta na kuhusisha maana ya neno geni katika lughamama, Kiswahili au lugha nyingine yoyote ambayo tayari tumejifunza. Maana ya dhana: kujifunza ndiyo imejikita hapo: kuweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya maneno au dhana mpya kutoka lugha ya kigeni na lugha zetu za awali. Tukiweza kujenga huo uhusiano ndiyo tumejifunza au tumeelewa maneno au dhana hizo katika lugha ya kigeni.


Nchini Marekani miaka ya 1980, kulitokea harakati ya kusisitiza matumizi ya Kiingereza pekee (English Only) kama lugha rasmi na ya kufundishia kwa kuwa ni lugha kuu ya taifa hilo. Hali hiyo ilitokana na baadhi ya watu wenye nafasi kuhisi kuwa Kispaniola kinanyemelea na kutishia Kiingereza, hasa katika maeneo ya kusini mwa nchi hiyo wanakopakana na Amerika ya Kusini ambako lugha kuu ni Kispaniola. Harakati hizo zilizimwa kwa jitihada za baadhi ya raia ikiwemo Chama cha Walimu wa Kiingereza kwa Wazungumzaji wa Lugha Zingine: yaani Teachers of English to Speakers of Other Languages, (TESOL). Chama hicho cha walimu kilisisitiza kuwa sera ya Kiingereza pekee haijengi Kiingereza, bali inazuia matumizi ya lugha zingine! Kwa maelezo ya Crawford (1992, 1997), kauli hiyo ya walimu hao iliwashangaza wengi kwa sababu wengi waliamini kuwa sera hiyo inakuza na kutetea (promote) Kiingereza; na kwa hiyo walimu hao walitarajiwa kuunga mkono harakati hizo. Jambo ambalo walimu hao wa Kiingereza walilielewa (ambalo wengi hawakulielewa) ni kwamba wanafunzi hao wanaozungumza lugha zingine wanahitaji lugha zao za awali kama msingi wa kujifunza Kiingereza; na ndiyo maana walipinga vikali harakati hizo za English Only. Hatimaye walimu hao walishinda kuzima harakati hizo kwa kuelewesha Umma, Senate na Serikali yao; na ikapitishwa kauli-mbiu ya English Plus... Other Languages; yaani wasijifunge katika Kiingereza pekee bali wakaribishe na kujifunza lugha zingine ili kukidhi mahitaji ya ulimwengu huu wa utandawazi. Iwapo Wamarekani wameona kuwa Kiingereza pekee haiwezi kutosheleza mahitaji ya ulimwengu wa leo, sisi Watanzania tunawezaje kuwa na sera inayotetea Kiingereza pekee na kukataza lugha zetu? Hapo tuna jambo la kujifunza.

Barani Afrika, (siyo sisi Tanzania peke yetu) sera hii ya kutumia lugha za kigeni pekee katika elimu kama vile English Only..., French Only..., au Portuguese Only imedumu hata baada ya nchi za Kiafrika kupata uhuru hadi sasa (Prah, 1994, 2003; Brock-Utne, 2012) na sera hii inayosisitiza matumizi ya lugha za kigeni haijaonesha kusaidia kuboresha ufundishaji wa lugha hizi. Kinyume chake sera hii imedhoofisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hizo; na sababu kubwa ni kwamba sera hii haijazingatia

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 30 06/07/2023 12:15 PM

hali halisi ya kujifunza na kufundisha lugha hizo za kigeni. Nchini Tanzania, sera hii ya kukataza matumizi ya lugha ya kwanza au lughamama katika shule za msingi na Kiswahili katika shule za sekondari inawafanya wanafunzi kutokuwa na kanuni (code) na msingi imara katika lugha yo yote; na kwa hiyo kuwa na mazingira finyu ya kusimika na kujifunza Kiingereza. Matokeo ya sera hii ni kwamba wanafunzi wa sekondari wamekosa umilisi wa lughamama, hawapati umilisi wa Kiswahili; na kwa hiyo wanakosa kumilisi Kiingereza kwa kuwa sera imeacha ombwe na hivyo kudhoofisha ufundishaji wa Kiingereza. Kielelezo 1 kifuatacho kinatoa picha ya hali halisi ya matumizi ya lugha nchini Tanzania (hasa maeneo ya vijijini) kuanzia mtoto anapozaliwa hadi umri wa miaka sita au saba; anapokwenda shule ya msingi umri wa miaka saba hadi 13; anapoingia sekondari hadi kumaliza chuo kikuu; na maisha baada ya kuhitimu, akiwa na ajira au bila ajira.

Kielelezo 1: Hali Halisi ya Matumizi ya Lugha katika Elimu na Jamii Nchini Tanzania



Kielelezo 1 kinaonesha hali halisi ya matumizi ya lugha nchini Tanzania na jinsi wanafunzi wanavyokatishwa kujifunza lugha yo yote wakafuzu vema; yaani kutoka lughamama kwenda kwenye Kiswahili; kutoka Kiswahili kwenda kwenye Kiingereza na hatimaye kutoka Kiingereza na kurudi tena kwenye Kiswahili. Kukatishwa huku, kama alivyosema Rubagumya (1997) miaka zaidi ya 20 iliyopita kunawakosesha wanafunzi msingi imara katika lugha yo yote kuanzia lughamama, Kiswahili na hata Kiingereza. Kielelezo hiki kinadhihirisha kwamba Kiingereza kinatumika tu katika elimu ya sekondari na vyuo vya juu kikiwa kimebebwa na sera; na kunatoa sura ya mchepuko wa miaka isiyopungua tisa (4 + 2 + 3); na kisha sehemu kubwa ya wahitimu wanarudi katika jamii inayotumia Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano wakiwa na uelewa finyu wa walichosomea na uwezo mdogo wa lugha ya Kiswahili kujieleza kwa jamii ya Watanzania. Hoja hii itajidhihirisha zaidi tutakapoangalia na kulinganisha hali halisi ya ufundishaji wa Kiingereza na matumizi ya lugha katika nchi zingine duniani (sehemu ya 4.0) na hali ya kwetu Tanzania. Kabla ya ulinganisho huo, ni vema tutazame matokeo ya hali halisi ya matumizi ya Kiingereza katika elimu nchini Tanzania.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 31 06/07/2023 12:15 PM

Matokeo ya hali halisi ya matumizi ya Kiingereza nchini Tanzania: Hali halisi ya ufundishaji wa Kiingereza kama tulivyoona hapo awali inaweka mazingira yanayokwamisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza. Mazingira hayo ni pamoja na: malengo ya kufundisha Kiingereza kutokuwa wazi; Kiingereza kutumika kufundishia; na kukataza matumizi ya lugha zingine. Hali hii imekuwa na madhara kadhaa ambayo ni pamoja na:

Sehemu kubwa ya mada zinazofundishwa kwa Kiingereza hazieleweki kwa wanafunzi waliowengi. Uelewa mdogo wa mada, kinyume/tofauti na uelewa mpana na wa kina unawafanya wanafunzi kushindwa kutumia lugha. Kazi kuu ya lugha ni kuwasilisha hoja ambayo tayari tumezijifunza na kuzielewa. Kama hakuna hoja ambazo tumejifunza au tumeelewa, tunalazimika kukaa kimya kwa sababu hatuna cha kutusukuma kutaka kutumia lugha. Lugha inapata kazi pale tu ambapo kuna cha kueleza na kushirikisha wengine. Kwa hiyo uelewa mdogo au finyu wa maarifa yanayofundishwa kwa Kiingereza hukwamisha pia uwezo wetu wa kujifunza Kiingereza na kukitumia Kiingereza kujieleza.

Utaratibu wa kukatisha matumizi ya lugha kutoka lughamama kwenda Kiswahili; kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na baadaya kutoka Kiingereza na kurudi kwenye Kiswahili (Kielelezo 1) unawanyima wanafunzi kuwa na msingi imara katika lughamama, Kiswahili na hata Kiingereza. Kutokuwa na msingi imara katika lugha za awali (lughamama na Kiswahili) kunawafanya wanafunzi kutojifunza lugha yoyote pamoja na Kiingereza kwa umahiri na umilisi kuliko kama wangekuwa na msingi aidha katika lughamama au katika Kiswahili.

Kukatika kwa mawasiliano kati ya wasomi wa Kitanzania na jamii pana ya Watanzania ni athari kubwa inayotokana na kusisitiza matumizi ya Kiingereza katika elimu na kukataza lugha zingine pamoja na Kiswahili. Kwa mfano sisi Tanzania, elimu yetu inasisitiza matumizi ya Kiingereza ilhali lugha kuu ya mawasiliano katika jamii pana ya Watanzania ni lugha za asili na Kiswahili. Kutofautiana huku kwa sera ya lugha katika elimu na hali halisi ya matumizi ya lugha katika jamii kumesababisha kukengeuka kwa wasomi wengi ambao wanashindwa kuwasiliana na jamii zao na kujihisi kuwa ni wageni wakirudi kijijini walikozaliwa kwa kuwa wamepoteza lugha zao za asili. Siku za usoni kuna uwezekano mkubwa baadhi ya watoto wa Kitanzania waliozaliwa na kulelewa hapa nchini wakawa hawafahamu Kiswahili kwa kuwa wazazi wao na mfumo wa elimu umekuwa unasisitiza matumizi ya Kiingereza tu.

Madhara mengine yanayotokana na hali hiyo ni ugumu wa kuwaandaa walimu waliofuzu bara bara katika kufundisha Kiingereza kama lugha. Kwa kuwa walimu hawa walikuwa katika mazingira ambayo kwa zaidi ya miaka sita walipokuwa wanafunzi, walisikiliza kwa muda mwingi walimu wanaotumia Kiingereza kisicho sahihi. Baada ya miaka hiyo sita, wanafunzi hao wanakuwa na miaka miwili (au mitatu) katika vyuo vya ualimu kujifuza mbinu za kufundisha Kiingereza ili wakafundishe katika shule za sekondari. Lakini, kwa kuwa hawakupata msingi imara wa lugha yoyote na wamekuwa wakisikiliza Kiingereza kisicho sahihi kwa miaka sita, inakuwa vigumu kwa miaka mitatu ya chuo kikuu kuwabadilisha kwa kuwatoa kwenye Kiingereza kibovu na kuwafundisha Kiingereza sahihi mpaka wawe wataalamu waliofuzu kufundisha Kiingereza. Kwa hiyo, kwa sasa juhudi kubwa inahitajika kuwaandaa walimu wa Kiingereza kuliko ambavyo ingekuwa kama wangejifunza Kiingereza kutoka kwa walimu walioandaliwa kuwa waalimu bora wa Kiingereza.

Madhara yanayotokea ni vigumu kuyaondoa au kuyarekebisha iwapo hatutabadilisha sera ya lugha na mazingira ya kufundisha Kiingereza katika shule za sekondari nchini Tanzania. Kabla ya kuzungumzia namna ya kubadilisha kwa kuboresha mazingira ya kufundisha Kiingereza nchini Tanzania ni vema kuzipitia nadharia ya kujifunza lugha ya pili au ya kigeni ili nazo zitupe mwongozo wa kufundisha Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni.

Nadharia zilimosimikwa Ufundishaji/Ujifunzaji wa Lugha ya Pili au ya Kigeni Nadharia ya Kizingiti (Threshold Theory): Nadharia ya hii (Cummins, 1979) inasema kwamba kuna vizingiti viwili ambavyo mtoto anayejifunza lugha mbili inabidi avivuke ili asipatwe na matokeo hasi ya kuwa na lugha mbili hafifu. Cummins, 1979 amenukuliwa na Baker and Hornberger 2001:18) kwamba kuna vizingiti hivi viwili ambavyo mtoto anayejifunza lugha mbili ni lazima avivuke ni kiwango maalumu cha umilisi wa lugha katika lugha zote mbili; yaani lugha ya kwanza na lugha lengwa – ya pili au ya kigeni. Katika nchi za Afrika zinazotumia Kiingereza, nadharia hii inahitaji mtoto awe na kiwango maalumu cha umilisi wa lugha ya kwanza kabla hajaanza kufundishwa Kiingereza. Kwa Tanzania, nadharia hii inahitaji wanafunzi wafikie kiwango maalum cha umilisi wa lugha ya Kiswahili kabla ya kuanza kujifunza Kiingereza. Umilisi wa lugha ya Kiswahili unawapa wanafunzi msingi (benchmark) imara

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 32 06/07/2023 12:15 PM

wa kujifunza Kiingereza. Hali hii itawawezesha wanafunzi kuwa na umilisi katika lugha zote mbili; kinyume chake, wanafunzi wanakosa umilisi wa lugha zote mbili; yaani Kiswahili na Kiingereza. Hali ambayo inaendelea sasa hivi.

Umilisi wa Msingi wa Pamoja (Common Underlying Proficiency): Cummins, (2000) aliboresha nadharia yake ya awali na kutoa hoja ya kuwepo kwa umilisi wa msingi wa pamoja baina ya lugha; na kusema kwamba maarifa aliyojifunza mwanafunzi kwa lugha moja huhamishika kwenye lugha nyingine na kujenga mazingira bora zaidi kuliko yote kwa lugha kufanya kazi bara bara. Cummins (2000) anasema kuwa: "Maarifa yaliyofikiriwa au kuundwa katika lugha moja (Lughamama) huwezesha maarifa yanayokuja kwa lugha zingine (lugha lengwa) kueleweka vema."('Conceptual knowledge developed in one language helps to make input in the other languages comprehensible.'). Anasema iwapo mtoto tayari anaelewa dhana ya "haki" au "uaminifu" katika lugha yake, anachohitaji kujifunza ni majina ya hizi dhana katika Kiingereza. Ila atakuwa na kazi ngumu zaidi iwapo atalazimika kujifunza kwa wakati mmoja majina na maana ya dhana hizi kwa Kiingereza. Katika mazingira ya shule za sekondari, Tanzania maana yake ni kwamba, jambo ambalo mwanafunzi amelielewa kwa Kiswahili (au lughamama) hahitaji kulijifunza upya kwa Kiingereza. Yaani, kuelewa ni kule kule kulikopatikana kwa lughamama au Kiswahili; na maarifa waliyojifunza wanafunzi kwa Kiswahili yanapanua wigo wa kujifunza Kiingereza. Cummins anaendeleza hii nadharia yake ya Umilisi wa Msingi wa Pamoja kwenye nadharia yake nyingine ya Kutengamana kwa Lugha.

Nadharia ya Kutangamana kwa Lugha (Language Interdependence Theory): Katika hatua nyingine (Cummins, 2001) anasema kuwa kuna utangamano kati ya lugha ya kwanza na lugha lengwa katika kujifunza lugha. Nadharia hii ya Cummins (2001) ya Kutangamana kwa Lugha inasema kwamba lugha anayojifunza mtoto kwanza, yaani lughamama, inajenga msingi imara wa kujifunza lugha zingine zinazofuatia. Anaendelea kusema: "Hatua ya juu ya maendeleo ya lugha inayofikiwa katika lugha ya kwanza inawezesha hatua hizo hizo za umilisi wa lugha kufikiwa katika lugha ya pili" ('...the initially high level of first language development makes possible the development of similar levels of competence in the second language'). Na kwamba kinyume chake ni kuwa: '...kwa watoto wale ambao ujuzi wao katika lugha zao za kwanza, kwa mfano lughamama au Kiswahili haujaendelezwa vema, kuwaingiza kwa bidii katika Kiingereza wakiwa madarasa ya awali kunaweza kukwamisha maendeleo endelevu ya lughamama na Kiswahili; hali ambayo itaathari na kukwamisha maendeleo yao katika Kiingereza. Kwa maelezo mengine, umilisi wao katika lughamama na Kiswahili huwawezesha kujenga umilisi wa kiwango hicho hicho katika Kiingereza. Hii ndiyo maana iliyokusudiwa katika nadharia ya kujifunza lugha ya kigeni au ya pili. Kwa hiyo, hakuna haja ya kupambanisha lugha au lugha moja kujaribu kuchukua nafasi ya lugha zingine. Kinachohitajika ni kupanua wigo wa mawasiliano uliojengwa katika lugha kadhaa. Nadhari nyingine inayozungumzia matumizi ya lugha katika jamii ni ile ya Philipson (1992), ambayo inajadiliwa katika sehemu inayofuata.

Nadharia ya Ubeberu wa Lugha (Linguistic Imperialism): Ubeberu wa Lugha inatokana na nadharia ya Galtung (1980) ya ubeberu kwa kuwa inajaribu kuunganisha vipengele kadhaa vya ubeberu na kwa hiyo kuruhusu ubeberu wa lugha kuwemo humo pamoja na aina nyingine za ubeberu. Ubeberu wa lugha ni sehemu ya alichokiita Galtung 'ubeberu wa kitamaduni'. Galtung (1980: 107) anafafanua ubeberu kuwa ni "aina ya mahusiano ambayo jamii moja (kwa pamoja au kwa ujumla wake) hutawala nyingine" ikiendeshwa kwa njia kuu nne: unyonyaji, upenyaji/uingiliaji, kuvunjavunja na kuwekwa ukingoni. Nadharia hii inafanya kazi kwa kugawa dunia katika maeneo yenye mamlaka (nchi zilizoendelea za Magharibi zenye nguvu pamoja na maslahi yao) na maeneo ya pembezoni yanayotawaliwa (nchi zisizoendelea). Kuna maeneo yaliyo na mamlaka kote katika nchi zilizoendelea na katika nchi za ukingoni. Maeneo ya ukingoni katika nchi zilizoedelea na zisizoendelea yananyonywa na maeneo yao husika yenye mamlaka. Tabaka la watu wenye uwezo katika nchi zilizoendelea na zisizoendelea wameunganishwa na maslahi ya pamoja (shared interests) ndani ya kila aina ya ubeberu. Kanuni ziwe za kiuchumi, kijeshi, au kiisimu zinaongozwa na wenye mamlaka katika nchi zilizoendelea na yamekaririwa na wenye mamlaka katika nchi za pembezoni.

Kwa maoni ya Galtung, katika awamu mwazo ya ukoloni, tabaka la watu wenye uwezo katika nchi za pembezoni/ukingoni ilikuwa ni wakoloni wenyewe. Katika ukoloni mamboleo wa sasa, tabaka lenye uwezo kwa kiwango kikubwa ni wenyeji; lakini wengi wao wana mahusiano mazito na wenye mamlaka katika nchi zilizoendelea. Wengi wa wenyeji wenye uwezo wamesomeshwa katika nchi zilizoendelea kwa lugha za nchi zilizoendelea, zile lugha za wakoloni. Katika awamu ya ukoloni mamboleo wa ubeberu, mashirika ya kimataifa yameshika nafasi muhimu. Kwa hiyo, Ubeberu wa Lugha unaweza kufafanuliwa kuwa ni hali ya lugha (ya mataifa makubwa) kujipenyeza katika nchi za pembezoni kwa maslahi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ya nchi zilizoendelea. Ni kutawaliwa kwa nchi za pembezoni kwa kutumia lugha.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 33 06/07/2023 12:15 PM

Philipson (1992) anatoa hoja kwamba ubeberu wa lugha unapenya na kusambaza aina zote za ubeberu kwa sababu; kwanza, lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano kwa mahusiano katika jamii zote. Lugha hasa ni sharti la kwanza kwa aina nyingi za mwingiliano ukiacha matumizi ya mabavu. Ni sehemu ya msingi ya ubeberu wa kitamaduni, ingawa usambazaji wa utamaduni unaweza kutumia njia zilizo nje ya lugha. Ubeberu wa lugha ni muhimu pia kwa ubeberu wa kijamii, ambayo inahusiana na kupitishwa kwa taratibu na tabia ya mfumo wa jamii unaokusudiwa na hizi zimebebwa na lugha. Philipson (1992) anakwenda mbali zaidi kuelezea kuwa nadharia ya ubeberu wa lugha inatupa mfumo wa dhana ambamo ndani yake Ubeberu wa Lugha ya Kiingereza unaweza kuelezewa; yaani kutawala kwa Kiingereza duniani kote na juhudi za kukipandisha daraja zinaweza kueleweka:

> ...kutawala kwa Kiingereza kunatetewa na kuendelezwa na wenye madaraka na kwa uundwaji endelevu usiosawa wa mara kwa mara wa kimfumo na kitamaduni kati ya Kiingereza na lugha zingine (Philipson, 1992: 4) (tafsiri yangu).

Uundwaji usiosawa wa kimfumo na kitamaduni unahakikisha mwendelezo wa utoaji wa rasilimali zaidi kwa Kiingereza kuliko lugha zingine na kuwanufaisha wale wenye umilisi katika Kiingereza ili waweze kupata rasilimali bora zaidi. Katika shule za sekondari Tanzania, Kiingereza kinapewa rasilimali muda kuliko Kiswahili, ingawa lugha yenye uwigo mpana wa kufanikisha mawasiliano ni Kiswahili. Uundwaji usio sawa wa kimfumo na kitamaduni unadhihirika katika shule zetu ambako sera inasisitiza matumizi ya Kiingereza, japo ni lugha inayoeleweka kwa wachache sana; na kwa wengi inakwamisha mawasiliano na hivyo wengi kukosa ujuzi na maarifa; na hata Kiingereza chenyewe. Kuwepo kwa msisitizo wa lugha ya Kiingereza katika nchi zilizotawaliwa na Waingereza kama Tanzania na Kiingereza kupewa nafasi na rasilimali kubwa zaidi kuliko lugha nyingine, kwa maelezo ya Philipson ni mwendelezo wa ubeberu wa lugha. Ni sehemu ya maslahi ya waliotutawala na siyo kwa maslahi ya nchi zetu. Sehemu inayofuata itaelezea kwa ufupi ufundishaji wa Kiingereza kama lugha ya kigeni katika nchi mbali mbali duniani zikiwemo za Ulaya na Asia.

Nchi zingine wanavyofundisha Kiingereza kama lugha ya kigeni

Ufundishaji wa Kiingereza katika Bara la Asia

Katika Bara la Asia nchi zinazofundisha Kiingereza kama lugha ya kigeni ni pamoja na Korea, Indonesia, Bangladesh, Thailand na nyinginezo. Nchi hizi zote na zingine zinatumia lugha za mataifa yao kufundishia shule za sekondari mpaka vyuo vikuu; na katika shule za msingi lugha za asili zinaruhusiwa kutumika kwa miaka miwili hadi mitatu ya kwanza ndipo wanahamia katika lugha za taifa. Nchi hizi zinafanana katika mambo yafuatayo:

a. Wanaweka malengo yaliyowazi na yanayotekelezeka yanayoafikiana (relevant) na mazingira yao
b. Wanatumia Lughamama kama msingi wa kufundisha na kujifunza Kiingereza; maana yake wanaweka maanani nadharia ya kujifunza na kufundisha lugha ya kigeni.
c. Wanatumia mifano halisi ya kwao ambayo inaeleweka vizuri kwa wanafunzi wao.
d. Wanatengeneza mazingira bora ya kujifunza na kufundisha kwa kuandaa vitabu vya kutosha vya ngazi mwafaka kwa kila hatua.
e. Wanatumia ufundishaji unaofikirisha; kwa mfano, aina ya maswali kama vile: Nini kitatokea ikiwa...? Na kwanini...? Wanahamasisha wanafunzi kuuliza maswali, kushirikishana, kushirikiana na wenzao maarifa waliyofahamu kwa kujifunza kwa lugha za awali. Kuwapa nafasi ya kujieleza kwa wenzake; utayari wa kufanya mazoezi, utayari wa kutumia lugha katika mazingira halisi ya darasa na shule, kujenga uhusiano kati ya wanayojifunza na yale wanayoishi.
f. Waalimu huzifahamu na kuzijaribisha njia mbali mbali za kufundisha na kuwa tayari kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji,
g. Waalimu huwafundisha wanafunzi kufanya uchambuzi yakinifu wa masuala mbali mbali wanayofundishwa.

Kwa kulinganisha hali halisi ya matumizi ya lugha, kile Kielelezo 1 kinachoakisi hali ya halisi ya matumizi ya lugha Tanzania, katika nchi tajwa za Asia wanafunzi wanahama mara moja tu, kutoka lughamama kwenda ya taifa ambayo wanaendelea nayo hadi vyuo vikuu na maisha baada ya kuhitimu. Wao hawapotezi lughamama, wanaimarisha lugha ya taifa na wanajifunza vizuri Kiingereza na lugha zingine za kigeni kama masomo la lugha. Elimu yao inasisitiza lugha zaidi ya mbili au tatu; na inajulikana kama multilingual education au 'elimu kwa lugha nyingi' kwa tafsiri nyepesi.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 34 06/07/2023 12:15 PM


Ufundishaji wa Kiingereza Bara la Ulaya

Ufundishaji wa Kiingereza kama lugha ya kigeni Barani Ulaya kwa nchi kama: Norway, Ufaransa, Italia, Ujerumani, Latvia, Slovakia, na zinginezo hautofautiani sana na tulivyoona katika Bara la Asia, ila wao wameboresha zaidi kwa kutumia vitabu vya kufundishia Kiingereza vikiwa na maelezo kwa lughamama zao.


Wanaweka malengo yaliyowazi na yanayotekelezeka yanayoafikiana (relevant) na mazingira yao. Wanatumia Lughamama kufundisha na kujifunza kutoka shule za awali, msingi na sekondari hadi vyuo vikuu bila kuhama hata mara moja. Kiingereza kinafundishwa kama lugha ya kigeni kwa misingi ya Lughamama; kwa hiyo maana yake wanaipa uzito kueleweka kwa kinachosemwa; na pia wanatilia maanani yanayoelezwa na nadharia ya kujifunza na kufundisha lugha za kigeni. Pia wanafanikiwa kujifunza lugha nyingine kadhaa za kigeni kwa kuwa wanamsingi imara wa Lughamama unaowawezesha kujifunza lugha zingine kwa wepesi. Wanatumia mifano halisi ya kwao ambayo inaeleweka vizuri kwa wanafunzi wao. Wanatengeneza mazingira bora ya kujifunza na kufundisha kwa kuandaa vitabu vya kutosha vya ngazi mwafaka kwa kila hatua. Kama wenzao wa Asia, nao pia wanatumia ufundishaji unaofikirisha; kwa mfano, aina ya maswali kama vile: Nini kitatokea ikiwa...? Na kwanini...? Wanahamasisha wanafunzi wao kuuliza maswali, kushirikishana, kushirikiana na wenzao maarifa waliyofahamu kwa kujifunza kwa lugha za awali. Kuwapa nafasi ya kujieleza kwa wenzake; utayari wa kufanya mazoezi, utayari wa kutumia lugha katika mazingira halisi ya darasa na shule, kujenga uhusiano kati ya wanayojifunza na yale wanayoishi. Waalimu huzifahamu na kuzijaribisha njia mbali mbali za kufundisha na kuwa tayari kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji. Waalimu huwafundisha wanafunzi kufanya uchambuzi yakinifu wa masuala mbali mbali wanayofundishwa.


Kwa kulinganisha hali halisi ya matumizi ya lugha na ufundishaji wa Kiingereza baina ya Tanzania (kuhamahama mara 3), Bara la Asia (kuhama mara moja) na Bara la Ulaya (hakuna kuhama) tutazame Kielelezo cha 2.

Kielelezo 2: Matumizi ya lugha katika Elimu na Jamii: Tanzania, Asia na Ulaya



Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 35 06/07/2023 12:15 PM





Tukilinganisha matumizi ya lugha na ufundishaji wa Kiingereza nchini Tanzania na nchi zingine za Bara la Asia na Ulaya kunatofauti kubwa sana. Kama inavyoonesha katika Kielelezo cha 2, Katika Bara la Ulaya Kiingereza kinafundishwa kama somo na masomo mengine yote yanafundishwa kwa lughamama kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu; kwa hiyo wanafunzi hawalazimiki kuhama kutoka lugha moja kwenda nyingine. Barani Asia Kiingereza kinafundishwa pia kama somo na lughamama inatumika kufundishia katika kipindi cha mpito (miaka 2 hadi 3 ya mwanzo) kisha wanafunzi wanahama mara moja tu kutoka lughamama kwenda kwenye lugha ya taifa kuanzia mwaka wa 3 au wa 4 wa shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Maamuzi yao ya kutumia lughamama au lugha ya taifa yanaongozwa au yamesimama katika nadharia ya kujifunza lugha. Kinyume chake sisi Tanzania hatuzingatii nadharia ya kujifunza/kufundisha lugha ya pili au ya kigeni; na matokeo yake wanafunzi wanahama siyo chini ya mara tatu: kutoka lughamama kwenda Kiswahili, kisha kwenda Kiingereza na hatimaye kurudi kwenye Kiswahili.

Kwa kufanya hivyo, tumeacha kuzingatia nadharia na hatujajifunza kutoka mabara mengine wanaofundisha Kiingereza kama sisi. Uwezo wao wa kuzungumza na kuandika Kiingereza na lugha zao unaelekea ni bora zaidi kuliko wetu; wakati sisi tunakosa ubora katika lughamama, Kiswahili na hatimaye katika Kiingereza. Kwa hiyo kuna jambo la kujifunza kutoka kwao. Moja

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 36 06/07/2023 12:15 PM

lililodhahiri ni kwamba wanapofundisha Kiingereza hawakatazi lugha zao, bali wanazitumia kama msingi wa kujifunza lugha za kigeni kama Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina, n.k. Wengi wetu wanadai kwamba nchi hizo zimeendelea ndiyo maana zinatumia lugha zao. Hiyo siyo sahihi, walitumia lugha zao na kupata maarifa kwa uhakika zaidi, ndipo maarifa hayo yakawawezesha kuendelea. Kwa hiyo, wakati mwingine wakitushauri (kama wanavyofanya mara nyingi) kwamba Kiingereza kifundishwe na kitumike kama lugha pekee (Criper and Dodd, 1984) tunawajibu wa kuwauliza iwapo wao wanapofundisha Kichina au Kiswahili, wanakataza lugha zao zisitumike.

Sera ya lugha katika nchi au jamii yo yote ni kufanya maamuzi na kupanga jinsi lugha mbali mbali za jamii zitakavyotumika. Sera ya lugha ni tamko la serikali kuhusu lugha gani ishike nafasi ipi katika jamii husika. Msingi wa tamko hili hujengwa katika kutambua umuhimu wa mawasiliano shirikishi na jumuishi katika jamii pana ya nchi au taifa husika. Hali hii (ya msingi wa sera ya lugha kujikita katika mawasiliano shirikishi na jumuishi) inajidhihirisha zaidi katika nchi zilizoendelea, ambako lugha kuu ya jamii ndiyo inayopewa nafasi na rasilimali zaidi ili lugha hiyo iweze kufanya vema kazi ya mawasiliano.
Barani Afrika, sera ya lugha haionekani kuzingatia umuhimu wa mawasiliano shirikishi na jumuishi baina ya jamii pana ya nchi au taifa husika za Kiafrika; bali inajenga tabaka la wasomi lenye kutumia lugha za kigeni; na tabaka la wasio wasomi ambao hutumia lugha za Kiafrika. Kwa jicho la haraka, sera hii ya lugha inaonekana kana kwamba inalenga kuleta maendeleo na mawasiliano ya kimataifa katika Bara la Afrika; lakini tunasahau kwamba mawasiliano ya kimataifa yanahitaji kutanguliwa na mawasiliano ndani ya taifa – kama hatua ya kwanza; na mawasiliano ya kimataifa, japo ni muhimu, ni hatua ya pili baada ya taifa kuwa na mawasiliano yanayoleta uelewa wa pamoja. Kufundisha na kujifunza lugha, kama ilivyo katika mambo mengi, ni vigumu kuanza kutekeleza hatua ya pili (mawasiliano na kuelewana na mataifa mengine) kabla ya kutekeleza hatua ya kwanza (mawasiliano na uelewa wa pamoja ndani ya taifa).

Kama inavyodhihirishwa katika hali halisi ilivyo sasa, ufundishaji wa lugha ya Kiingereza utaendelea kudhoofishwa kwa kuwa Kiingereza kinatumika kufundishia masomo mengine pasipo kujali usahihi na ufasaha; na pia kwa wanafunzi kukosa msingi (imara) wa lugha za awali (lughamama na Kiswahili). Kwa hiyo, ili kuboresha ufundishaji wa Kiingereza, jambo la kwanza ni kujenga mazingira bora ya kufundisha Kiingereza ikiwa ni pamoja na kufanya walimu wa Kiingereza waliofuzu vizuri kuwa chanzo pekee cha kujifunza Kiingereza (japo ni finyu) na kukiondoa Kiingereza kwenye nafasi ya lugha ya kufundishia; kuruhusu matumizi ya lugha zingine ili kuweka zazi maeneo yenye tofauti; na kuweka wazi malengo ya kufundisha Kiingereza. Baada ya kufanya haya mabadiliko ndiyo suala la kuboresha ufundishaji wa Kiingereza na mbinu gani zitumike linazungumzika.

Nini tutarajie baada ya kujifunza kwa wenzetu na kujua nadharia

Iwapo Tanzania tutakuwa tayari kujifunza kutoka nchi zingine na pia kuzingatia maelekezo ya nadharia ya kufundisha/kujifunza Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni, tunaweza kutarajia hali chanya zaidi ya kujifunza Kiingereza vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa.

Hali hiyo itawezekana iwapo sera ya lugha itaweka maanani umuhimu wa kuchagua lugha ya jamii pana kuwa ndiyo lugha ya kufundishia ili kuruhusu lugha ifanye kazi yake kuu ya kuwezesha MAWASILIANO. Naliwekea hili msisitizo kwa sababu ndiyo kazi kuu ya lugha, yaani kufanikisha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi na walimu au wanafunzi wenyewe kwa wenyewe. Uamuzi huu ukifanyika, itawezesha sehemu kubwa ya maarifa na ujuzi utakaofundishwa kwa Kiswahili kuwasilishwa na kueleweka kwa wanafunzi waliowengi. Uelewa huo mpana na wa kina (kinyume na uelewa mdogo wa sasa) watakaoupata wanafunzi utawawezesha kutumia Kiingereza kuelezea hayo maarifa kwa wenzao au kwa walimu wao (hata kama ni kwa Kiingereza kibovu). Kama nilivyoeleza awali kazi kuu ya lugha ni kuwasilisha kwa watu wengine mambo ambayo tayari tumeyajifunza na kuyaelewa; maana yake ni kwamba, kama hakuna ambacho tumejifunza au tumeelewa, tunalazimika kukaa kimya kwa sababu hatuna cha kutusukuma kutaka kueleza kwa wengine. Kwa hiyo, uelewa mdogo au finyu wa maarifa yanayofundishwa kwa Kiingereza hukwamisha pia uwezo wetu wa kutumia Kiingereza kujieleza. Tutakapotumia lugha inayoeleweka kwa wengi kufundishia; na kuruhusu matumizi ya lugha zingine kujifunza maarifa, uelewa mpana na wa kina tutatupa uwanja mpana wa kufanyia mazoezi Kiingereza na tutakijifunza vizuri.

Iwapo sera ya lugha itazingatia na kuweka maanani misingi ya nadharia ya kujifunza lugha itawezesha wanafunzi kuwa na msingi imara katika lughamama, katika Kiswahili; na hata Kiingereza. Kuwa na msingi imara katika lugha za awali (lughamama na

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 37 06/07/2023 12:15 PM

Kiswahili) kutawawezesha wanafunzi kujifunza lugha yo yote pamoja na Kiingereza kwa umahiri na umilisi huo huo wa lugha za awali. Hali hii ya kutumia lughamama inaungwa mkono na nadharia zilizojadiliwa katika makala hii pamoja na uzoefu katika nchi za Asia na Ulaya.

Wengi hudai kwamba Ulaya wanatumia lugha zao kwa sababu wameendelea; uzoefu na nadharia ya kujifunza na kufundisha lugha zinaonesha kuwa nchi hizo walitumia lugha zao ndiyo maana waliendelea! Boorstin (1983) anaeleza jinsi nchi za Ulaya zilivyoendelea Karne ya 18 baada ya kubadilisha lugha ya kufundishia kutoka Kilatini kwenda kwenye lugha zao kama vile: Kifaransa, Kiitaliano, Kiingereza, Kidachi, Kijerumani, n.k. Hata nchi za Kusini Mashariki mwa Asia walianza kushuhudia maendeleo ya ndani baada ya kuacha kutumia Kiingereza miaka ya 1960 hadi 1970 na kuhamia katika lugha zao. Hali hii inaonesha kwamba maendeleo ya jamii yo yote hutanguliwa na uelewa wa pamoja wa jamii kwa kutumia lugha inayoeleweka kwa wengi. Nchi hizi zote watu wao wanajifunza Kiingereza kama lugha ya ziada, siyo lugha mbadala kama sisi tunavyofanya. Katika Bara la Ulaya au Asia hakuna nchi ambayo imeacha lugha yake (zake) na wamejifunza Kiingereza kama lugha ya nyongeza kwenye lugha zao. Kwa hiyo hawajapata tatizo la kukatika kwa mawasiliano kati ya wasomi na jamii zao, kama sisi wasomi wa Afrika tunavyoelekea kukata mawasiliano na jamii zetu hapa Tanzania.

Kuhusu ufundishaji wa Kiingereza katika shule za sekondari nchini Tanzania, Kirkland (1976) anayo haya ya kusema:

> *Much time is now wasted in teaching the wrong kind of English to the wrong people and doing it badly so that a great deal of remedial work is needed before the language can be useful (Kirkland, 1976:114)*
> Akimaanisha: muda mwingi sasa hupotezwa katika kufundisha aina mbovu ya Kiingereza kwa watu ambao siyo na kufundishwa vibaya kiasi kwamba kazi kubwa ya marekebisho huhitajika kabla ya lugha kuweza kufaa. (Tafsiri yangu).

Katika hali ya sasa tunahitaji juhudi kubwa zaidi kuwaandaa walimu wa Kiingereza kuliko ambavyo wangetumia Kiswahili na siyo Kiingereza kibovu kinachotumika kufundishia. Madhara haya yanayotokea sasa ni vigumu kuyaondoa au kuyarekebisha iwapo hatutabadilisha sera ya lugha na mazingia ya kufundisha Kiingereza katika shule za sekondari nchini Tanzania.

Kwa kuwa lengo kuu la makala hii ilikuwa ni kujadili kuboresha ufundishaji wa Kiingereza; ni vema tufike mahali tujiulize kwanini sisi tunashindwa na wenzetu wanafanikiwa. Kikubwa na cha wazi ni kwamba wenzetu wa nchi zingine wanatilia maanani nadharia za kufundisha na kujifunza lugha ya pili au ya kigeni kama ilivyooneshwa hapo awali. Nadharia ya Kizingiti na Kutangamana kwa lugha zinaruhusu na kuhimiza matumizi ya lugha za awali tunapofundisha Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni ili kuipa Kiingereza msingi imara. Nadharia ya Umilisi wa msingi wa pamoja pia inasisitiza matumizi ya lughamama na lugha za awali, kwa hoja kwamba maarifa au ujuzi uliojifunzwa kwa lugha hizi za awali huhamishika katika lugha ya Kiingereza. Iwapo maarifa yanahamishika kutoka lugha moja hadi nyingine, basi kwa mantiki hiyo, lughamama ni bora zaidi kuchotea maarifa na ujuzi ili tukishayachote yawe ni uwanja wa kufanyia Kiingereza mazoezi – kwa kuwaeleza wengine maarifa hayo kwa Kiingereza. Kinyume chake, iwapo hatujapata maarifa wala ujuzi, tutakosa uwanja wa kujifunzia Kiingereza. Kwa hiyo njia moja kuu na muhimu ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza ni kukiondoa kama lugha ya kufundishia na kukifundisha kama somo la lugha, kama tunavyofundisha Kifaransa au Kichina kwa sasa. Nadharia ya ubeberu wa lugha inaonesha jinsi gani lugha za mataifa yaliyotutawala zinavyopewa kipaumbele na kupata rasilimali nyingi zaidi kuliko lugha za asili na lugha za taifa katika Bara la Afrika; na jinsi gani ili kujikomboa tunahitaji kuzielekeza rasilimali za nchi katika maeneo yanayoleta tija kwa jamii za Kiafrika kama vile elimu. Kwa hiyo, ni muhimu tunapozungumzia kuboresha ufundishaji wa Kiingereza (lugha lengwa) kuzingatia na kuweka maanani uwepo wa lugha zingine kama vile lugha za asili na Kiswahili ili kupata uelewa ambao utasaidia katika kujifunza Kiingereza.

Hitimisho

Katika makala hii tulijadili matatizo yanayokabili ufundishaji wa lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari nchini Tanzania hivi sasa. Matatizo hayo tulisema ni: kutowekwa maanani maelekezo ya nadharia za kufundisha/kujifunza lugha ya pili au ya kigeni; na sera ya lugha katika elimu kutozingatia suala la kufanikisha mawasiliano wakati wa kupanga na kuamua lugha ipi itumike kufundishia. Matatizo haya mawili yameonesha kuzaa mazingira ya kukwamisha badala ya kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza. Mazingira hayo ni pamoja na malengo yasiyo wazi na yasiyotekelezeka, matumizi ya Kiingereza kibovu

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 38 06/07/2023 12:15 PM

kutoka kwa walimu wasiofuzu vizuri Kiingereza, kukatazwa matumizi ya lugha zingine na kuwepo kwa vitabu vya ngazi isiyo mwafaka kwa wanafunzi wetu. Pamoja na mambo haya, makala hii pia imezipitia nadharia kadhaa zinazoongoza ufundishaji wa lugha ya pili au ya kigeni; na imelinganisha ufundishaji wa Kiingereza Tanzania na katika nchi zingine zinazofundisha Kiingereza kama lugha ya pili au ya kigeni. Makala pia imezungumzia athari za hali inayoendelea hivi sasa katika kufundisha Kiingereza na namna ya kukabili athari hizo kwa kuzingatia matumizi ya Kiingereza katika jamii pana ya Tanzania. Makala imetoa hitimisho kwa kujadili njia mbali mbali zinazoweza kutumiwa ili kuboresha ufundishaji wa Kiingereza na kupendekeza njia zipi zitumiwe. Makala pia himiza mabadiliko ya sera ya lugha ili iweke maanani umuhimu wa jamii nzima ya Tanzania kuwa na lugha ya elimu ambayo ni lugha kuu katika jamii ili kuwezesha mawasiliano na uelewa wa pamoja ambao ni muhimu kwa uhai na maendeleo ya Taifa. Kwa mfano, karibu shule zote za sekondari nchini Tanzania zinafundisha kutumia Kiingereza; lakini kuna shule chache zinazofundishia Kifaransa kuanzia chekechea hadi sekondari. Hizi lugha mbili ni lugha za kigeni; kwanini tusiwe na shule (hata moja ya mfano) ambayo hufundisha kwa Kiswahili kuanzia chekechea hadi chuo kikuu? Kama tunaruhusu lugha za kigeni, kwanini tusiruhusu lugha kuu ya mawasiliano nchini mwetu kuwa lugha kuu ya elimu yetu?

Mapendekezo

Baada ya kujadili kwa namna ya kuboresha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza nchini Tanzania, napendekeza mambo yafuatayo:

Watunga sera waweke maanani maelekezo ya Nadharia za kujifunza na kufundisha lugha ili waweze kufanya maamuzi sahihi ya kisera

Mipango na maamuzi ya sera ya lugha katika elimu itilie maanani na kuzingatia kuwepo kwa nadharia za kujifunza na kufundisha lugha ya pili na ya kigeni ili kujiweka sawa na wenzetu wa nchi zingine. Nadharia hizi zituongoze katika kuchagua lugha yenye uwezo wa kuwasilisha ujuzi na maarifa kwa walengwa.

Kufundisha Kiingereza vizuri kama lugha ya kigeni na kisitumike kufundishia

Kufundisha Kiingereza vizuri kama lugha ya kigeni na kukitoa kwenye nafasi ya lugha ya kufundishia kutasaidia mambo kadhaa; mosi, kutapunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya Kiingereza kibovu katika mazingira ya shule; na pia kutasaidia katika maandalizi ya walimu wa Kiingereza; na kuwarudishia walimu hao wa Kiingereza mamlaka ya kuliendeleza somo lao kwa jinsi watakavyofunzwa. Pia kuondoa Kiingereza kama lugha ya kufundishia kutapunguza suala la kuhamahama kutoka lugha moja hadi nyingine katika mfuimo wa elimu na jamii pana. Kiingereza nchini kinatumika na watu wachache, matumizi yake katika kufundishia kunawakengeua wasomi na jamii zao. Hoja hii inaunga mkono nadharia za kujifunza/kufundisha lugha ya pili au ya kigeni na pia inakwenda sambamba na uzoefu wa kufundisha lugha hiyo katika nchi zingine.

Serikali ianzishe shule ya mfano itakayofundisha kwa Kiswahili kuazia chekechea hadi chuo kikuu

Baada ya kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia kwa miaka 60 ya Uhuru wa nchi yetu, bila kupata mafanikio ya kuridhisha katika ufundishaji wa lugha hiyo, Serikali itambue umuhimu wa kufanya jambo tofauti la kuanzisha shule ya mfano itakayofundisha kwa Kiswahili kuanzia chekechea hadi chuo kikuu; ambapo lugha kadhaa kigeni zitafundishwa vizuri na walimu waliofuzu kufundisha lugha hizo.

Matumizi ya lugha zingine yaruhusiwe

Sheria inazotumika shuleni kusisitiza Kiingereza Pekee ("English Only") haisaidii kuimarisha Kiingereza, bali inazuia matumizi ya lugha zingine. Nadharia ya kufundisha na kujifunza lugha na uzoefu kutoka nchi zingine hazikubaliani na sheria hii; pia nje ya Bara la Afrika, kwa uelewa wangu, sheria hii haitumiki mahali popote. Inapendekezwa hapa kuwa lugha zingine ziruhusiwe kutumika katika elimu kwa kuwa kila lugha ni nyenzo ya kubeba na kuwasilisha maarifa. Kwa mfano lughamama zitumike kwa miaka miwili au mitatu ya kwanza katika mfumo wa elimu.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 39 06/07/2023 12:15 PM

Ufundishaji wa Kiingereza usimame wenyewe ujitegemee

Kama ilivyo kwa masomo mengine, ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza usijitegemeze kwenye lugha ya kufundishia, bali ujitegemee wenyewe. Kudhani kuwa wanafunzi watajifunza Kiingereza wakiitumia kama lugha ya kufundishia na kujifunzia ni sawa na kutafuta njia ya mkato; na ni njia ya kukwamisha ujifunzaji wa lugha hiyo. Kama masomo mengine yanavyojitegemea na wataalamu wake na iwe hivyo kwa Kiingereza; Walimu wa Kiingereza wajitafakari na kutambua kuwa ni wajibu wao kufundisha vizuri bila kuwategemea walimu wa masomo mengine ambao Kiingereza siyo eneo lao la taaluma.

Walimu wa Kiingereza wafanyiwe mafunzo maalumu

Walimu wa Kiingereza wapate mafunzo ya kuwanoa vizuri kitaaluma ili waweze kufundisha Kiingereza kwa ufanisi zaidi.

Vitabu vya ngazi mwafaka viandaliwe

Vitabu vingi vya sasa ni vigumu kuvielewa kwa wanafunzi wengi wa Tanzania; kuna umuhimu Taasisi ya Elimu ipitie upya vitabu vya Kiingereza na kuandaa vya ngazi mwafaka ikizingatiwa kuwa kwa wanafunzi wengi wa Tanzania, Kiingereza ni lugha ya kigeni na siyo lugha ya pili.

Haya ni baadhi ya mapendekezo ya kusaidia kuboresha ufundishaji wa Kiingereza nchini Tanzania. Nina imani kuwa kuna njia nyingi kuliko hizi za kuboresha ufundishaji wa lugha hii hapa kwetu. Itoshe tu kusema kwamba hii makala ni kichocheo tu cha kuamsha ari ya kufundisha lugha hii pendwa hapa nchini kwetu Tanzania.

MAREJELEO

Baker, C. and N. Hornberger, (Eds.) (2001). An Introductory Reader to the Writings of Jim Cummins, Clevedon: Multilingual Matters.

Boorstin, Daniel J. (1983). The Discoverers, New York: Random House.

Brown, H. D. (2000). Principles of Language Learning and Teaching, Englewood Cliff, N.J.: Prentice Hall.

Brock-Utne, Birgit, 2006. Learning through a familiar language versus learning through a foreign language – a look into some secondary school classrooms in Tanzania. In Brock-Utne, B., Desai, Z., and Qorro, M. A.: LOITASA: Focus on fresh data on the language of instruction debate in Tanzania and South Africa, Cape Town: African Minds.

Brumfit, Christopher J. (1980). Problems and Principles in English Teaching, Oxford: Pergamon Press.

Crawford, Jim (1992a). Hold your tongue: Bilingualism and the politics of "English Only," Reading, MA: Addison-Wesley.

Crawford, Jim (1992b). What's behind official English? In J. Crawford (Ed.), Language loyalties: A source book on the Official English controversy (pp. 171-177), Chicago: University of Chicago Press

Crawford, Jim (1997). Best evidence: Research foundations of the Bilingual Education Act, Washington, DC: National Clearinghouse for Bilingual Education.

Cummins, J. (1979). 'Cognitive/Academic Language Proficiency, Linguistic Interdependence, and the Optimal Age Question and Some Other Matters' Working papers on Bilingualism, 19, 197-205.

Cummins, J. (1981). The Role of Primary Language Development in Promoting Educational Success for Language Minority Students', in Schooling and Language Minority Students: A theoretical Framework, 3-49.

Cummins, J. (2000). Language, Power and Pedagogy: Bilingual Children in the Crossfire, Clevedon: Multilingual Matters.

Cummins, J. (2001). An Introductory Reader to the Writings of Jim Cummins, in Baker, C. and N. Hornberger, (Eds.) (2001). Clevedon: Multilingual Matters.

Einarsson, (2001), 'Democracy and the Choice of Language of Instruction in Tanzania' a research paper, University of Uppsala, Sweden.

Eckart Harold, (2005). Quoted in Diana Rumpite in 'Cherishing Language Diversity in Latvia: European Day of Languages', in International Federation of Language Teachers Associations, World News, No. 62, May 2005.

Kadeghe, Michael (2000). 'The Implications of Bilingualism in Learning and Teaching: the Case of Tanzanian Secondary Schools'. Unpublished Ph.D. Thesis. University of Dar es Salaam.

Kirkland, B. G. (1976). The Language of Self-Reliance: Swahili Medium Secondary Education in Tanzania, in African Language

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 40 06/07/2023 12:15 PM

Journal No. 2, 105-117.
Mcha, Y. and E. Mrindoko (1980). Output from Schools, in Language for Education, Papers compiled by the Communication Skills Unit in the Department of Foreign Languages and Linguistics, University of Dar es Salaam.
Mlama, Penina na May Matteru (1978). 'Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Elimu ya Juu'. a research report commissioned by BAKITA. Dar es Salaam, Tanzania.
MoEC (1995). The Tanzania Education and Training Policy. Dar es Salaam.
Mvungi, Martha (1982). 'The Relationship between Performance in the Instructional Medium and Some Secondary School Subjects in Tanzania'. Unpublished Ph.D. Thesis. University of Dar es Salaam.
Mweteni, Y. (1996). 'Error Analysis with Special Reference to Tanzanian Learners of English', in the Journal of Linguistics and Language in Education, Journal of the Department of Foreign Languages and Linguistics, University of Dar es Salaam.
Mwinsheikhe, Halima (2007). 'Overcoming the Language Barrier: an In-Depth Study of Tanzanian Secondary School Science Teachers' and Students' Strategies in Coping with the English/Kiswahili Dilemma in the Teaching/Learning Process'. Ph.D. Dissertation. Faculty of Education, University of Oslo.
Phillipson, R. (1992). Linguistic Imperialism. Oxford: Oxford University Press.
Prah, K. (1994). Mother Tongue for Scientific and Technological Development in Africa, Bonn: ZED.
Prah, K. (2003). Going Native: Language of Instruction for Education, Development and African Emancipation, in Brock-Utne, B., Desai, Z. and Qorro, M., Language of Instruction in Tanzania and South Africa, Dare es Salaam: E & D Ltd.
Qorro, Martha A. S. (2005). 'Parents' Views on the Language of Instruction in Secondary Schools'. In Brock-Utne, B., Z. Desai and M. Qorro (Eds.). LOITASA Research in Progress. Dar es Salaam: KAD Associates.
Qorro, Martha A. S. (2008). 'A Review of Literature on the Language of Instruction Research in Tanzania'. In Qorro, M., Z. Desai and B. Brock-Utne. LOITASA: Reflecting on Phase I and Entering Phase II. Dar es Salaam: E & D Limited.
Qorro, Martha A. S. (2010) 'Testing students' ability to learn through English during the transition from primary to secondary schooling' in Brock-Utne, Desai, Z., Qorro and Allan Pitman, (Eds.), Language of Instruction in Tanzania and South Africa – Highlights from a Project, Sense Publishers: Rotterdam/Boston/Taipei. Comparative International Education, Vol. 5.
Qorro, Martha, A. S. (2011) 'Challenges of Teaching English in Africa: With Reference to Tanzania Public Secondary Schools', in UTAFITI, Journal of the College of Arts and Social Sciences, University of Dar es Salaam. Vol. 7 No. 2, pp. 35-52.
Qorro, Martha A. S. (2012) 'Investing in English Language Teaching from the Early Grades in Tanzania Primary Schools: In response to the recently proposed Language in Education Policy', in Qorro, Desai, and Brock-Utne (eds.), LOITASA: Understanding What the Teacher is Saying', KAD Associates: Dar es Salaam.
Qorro, Martha A. S. (2013) 'Language Planning and Policy in Tanzania: When practice does not make perfect', in Desai, Qorro and Brock-Utne (eds.) The Role of Language in Teaching and Learning Science and Mathematics, African Minds, Cape Town, South Africa.
Robert B. Kaplan and Richard B. Baldauf, Jr. (1997). Language planning: from practice to theory, Clevedon: Multilingual Matters Ltd.
Roy-Campbell, Zaline Makini (2001). Empowerment through Language – The African Experience: Tanzania and Beyond. Asmara: Africa World Press, Inc.
Roy-Campbell, Zaline Makini and Martha Qorro (1987). 'A Survey of the Reading Competence in English among Secondary School Students in Tanzania'. A Research Report funded by IDRC.
Roy-Campbell, Zaline Makini and Martha Qorro (1997). The Language Crisis in Tanzania: the Myth of English versus Education. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
Rubagumya, Casmir M. (Ed.) (1990). Language and Education in Africa: A Tanzanian Perspective. Philadelphia: Multilingual Matters.
Rubagumya, C. (1997), 'Disconnecting Education: Language as Determinant of the Quality of Education, (New Series), in Journal of Linguistics and Language in Education, (New Series), Vol. 3 pp. 81-93.
Rubagumya, Casmir, Kathryn Jones and Hermas Mwansoko (1999). 'Language for Learning and Teaching in Tanzania'. Unpublished ODA funded Research Report. Dar es Salaam.
Rubagumya, Casmir (2003). 'English Medium Primary Schools in Tanzania: a New "Linguistic Market" in Education?' In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai and Martha Qorro (Eds.). Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA). Pp. 149-170. Dar es Salaam: E & D Limited.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 41 06/07/2023 12:15 PM

Rugemalira, J. and Muzale, H. (2009). The Language Atlas of Tanzania, Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (2008). "English is not our motherland": Anecdotal discussions and views on the language question in Tanzania, in Qorro, M. Desai, Z. And Brock-Utne, B. LOITASA: Reflecting on Phase I and entering Phase II, Dar es Salaam: E&D Vision Publishing Limited.

Simmonds, P., C. Kivanda and C. Kazaura (1991). 'English Language Teaching Support Project: Project Monitoring Report'. Dar es Salaam: Ministry of Education/ODA.

Tume ya Rais (1982). 'Mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981-2000.' Juzuu la Kwanza. Dar es Salaam

.Tume ya Rais (1983). 'Mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981-2000'. Juzuu la Kwanza. Dar es Salaam.

UNESCO, 2005: First Language First: Community-based Literacy Programmes for Minority Language Contexts in Asia. Bangkok: UNESCO Bangkok.

UNESCO (2013). Handbook on Education Policy Analysis and Programming. Volume 1 Education Policy Analysis Bangkok: UNESCO.

URT (1995). Education and Training Policy Dar es Salaam: The Ministry of Education and Culture, Dar es Salaam.

URT (2005). 'Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 1995 -2005'. MoEC. June. Dar es Salaam.

Vuzo, Mwajuma (2005). 'Using English as a Medium of Instruction in Tanzania Secondary Schools: Problems and Prospects'. In Brock-Utne, B., Z. Desai and M. Qorro (Eds.). LOITASA Research in Progress. Dar es Salaam: KAD Associates.

Vuzo, Mwajuma (2007). 'Revisiting the Language of Instruction Policy in Tanzania: a Comparative Study of Geography Classes Taught in Kiswahili and English'. Ph.D. Dissertation. Faculty of Education, University of Oslo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2009). Sera ya Elimu na Mafunzo 2009. Rasimu ya I. Toleo Jipya, Juni, 2009.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2015). Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo. Rasimu ya I. Toleo Jipya, Februari, 2015.

Wolff, E. (2000), 'Indigenous Languages in Education: Learning from West African Experiences', a paper in the Proceedings of the Second National Symposium on Language Policy Formulation, in Joachim Friedrich Pfaffe, Mallawi: Mangochi.

Yahya-Othman, S. (1992). Science and Language in Tanzania: Weapons in the Empowerment Process, in Journal of Linguistics and Langauge in Education Vol. 6, pp. 1-19.

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 42 06/07/2023 12:15 PM

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 43 06/07/2023 12:15 PM

HakiElimu enables citizens to make a difference in education and democracy

P. O. Box 79401 | Dar es Salaam | Tanzania
Tel +255 22 2151852 / 3 | Fax. +255 22 2152449
info@hakielimu.or.tz | www.hakielimu.or.tz

Final Chapisho la Lugha ya Kufundishia-Booklet-JUSTFIED-Garamond.indd 44 06/07/2023 12:15 PM